ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tatu - Tarehe 12 Mei, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya Mwaka 2015.

Mhe. Suleiman Makame Ali (Kny. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Spika, ahsante sana kwa niaba yako na kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum. Mhe. Spika, naomba kuweka mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya Mwaka 2015.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2014/2015, na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf (Kny. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*): Mhe. Spika ahsante, kwa niaba yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Kamati ya *PAC* kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara na

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 49

Utaratibu Unaotumiwa na SMZ Kupata Fursa na Ufadhili wa Wahisani Kutoka Muungano

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:

Kwa kuwa afya, maji na elimu sio mambo ya Muungano.

Je, utaratibu gani unaotumiwa na SMZ kuhakikisha kuwa fursa na ufadhili kutoka nchi wahisani tunazipata.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammd Said swali lake Nam. 49 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli masuala ya afya, maji na elimu isipokuwa elimu ya juu si masaula ya Muungano na yanatekelezwa kupitia Sera, Sheria na taratibu za upande husika wa Muungano. Katika hali ya kawaida serikali husika ina jukumu la kuhakikisha kuwa inatafuta fursa za ufadhili kutoka nchi wahisani na mashirika mbali mbali ya kikanda, kimataifa ya kusaidia sekta hizi.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya miradi katika sekta hizo inakuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajumuisha Zanzibar, serikali zetu kupitia vikao mbali mbali vya utatuzi wa hoja za Muungano, hoja za mgawanyo wa mapato ya misaada na uwezo wa Zanzibar kukopa imejadiliwa kwa kina ambapo imekubaliwa kuwa Zanzibar itaendelea kupata mgao wake wa asilimia 4.5 kwa kila msaada au ufadhili unaokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, aidha serikali zetu mbili zinatumia utaratibu wa vikao vya ushirikiano wa kisekta kwa kila wizara kwa mambo yasio ya Muungano kwa lengo la kubadilishana ujuzi, sera, utaalamu na wataalamu pamoja na kutatua changamoto zilizopo katika sekta na majukumu yao.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante na mimi ningependa kumuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwa kuwa jana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Makamu mwenyewe alikiri pia kwamba katika ziara ambazo viongozi wa kitaifa hufanya ndani ya Jamhuri pia zimekuwa viongozi hawa hawafiki Zanzibar, lakini kutokana na umuhimu wake alikiri pia changamoto zilizokuwepo ndani yake na kutokana na historia na mila ambazo tulikuwa tukiendeleza katika miaka ya nyuma.

(a) Je, ni utaratibu upi sasa rasmi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais watajipangia rasmi ambao utakaotambulika wa Kikatiba na Kisheria ambapo utaweza kuisaidia katika mambo muhimu ambayo si ya Muungano kama elimu, afya na maji. Fursa ambazo zitaweza kuwasaidia Mawaziri wetu wanapotoka ndani ya Zanzibar kuwa sasa wana hadhi na Mawaziri kama wa Jamhuri ya Muungano, kwa sababu ndani ya nchi yetu tuna Mawaziri wa Zanzibar na Mawaziri pia wa Jamhuri.

Mhe. Spika: Mheshimiwa swali.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika.

(b) Kwa kuwa hata miaka ya nyuma tumeona Mawaziri ambao wanasimamia maeneo ya wizara ambazo sio za Muungano kufika pahala, na pia kuita hii ni Jamhuri na Muungano wetu ni Muungano wa Jamhuri ya Watu wa Zimbabwe pamoja na Pemba. Je, Mawaziri kama hawa wa Muungano wanaokosea na kufanya makosa haya makubwa kabisa, ni utaratibu gani wa kinidhamu Zanzibar inawachukulia katika hatua hii. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza

Mhe. Simai Mohammed Said kama ifuatavyo, lakini naomba nianze na hili la pili.

Mhe. Spika, samahani naomba arudie, itakuwa sijalifahamu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa yarejee maswali kwa ufupi sana yale maswali yenyewe usitoe maelezo mengi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante. Swali langu la (a) ni hivi:

(a) Nimeeleza kwamba jinsi jana Makamu wa Pili alivyokiri juu ya viongozi wa taifa. Ni utaratibu gani wa kisheria na Kikatiba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais watajipangia ili kuhakikisha Mawaziri wa Zanzibar pamoja na yeye mwenyewe akiwa Naibu Waziri sawa, wanakuwa na hadhi sawa sawa katika maeneo ambayo si ya Muungano pale wanapotoka nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Kwa kuwa huko nyuma Naibu Waziri wa Elimu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikiri kwenye mkutano akitoa hoja akasema kwamba, Muungano wetu huu ni Muungano wa Pemba na Zimbabwe, ambapo pia akataja kuwa wameungana mwaka 1964, mpaka mwaka alikosea. Ni hatua gani za kinidhamu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanawachukulia viongozi kama hawa ambao wanafanya makosa makubwa kabisa ya nchi. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi anauliza ni utaratibu gani tunaotumia.

Kwanza tumwambie tu ni utaratibu wa serikali zote duniani tukimzungumzia Waziri katika *level* yake, katika *jurisdiction* yake na anapotoka nje ya *jurisdiction* yake ataendelea kubaki kuwa Waziri, *no longer* kwamba wapo kwenye *union* ya aina yoyote. Waziri atabaki kuwa Waziri ndani ya serikali yake, atakapotoka katika taifa moja atatoka na *status* yake na akienda katika taifa la pili ataendelea ku-*maintain status* yake ya utaifa.

(b) Ni hatua gani za kinidhamu ambazo Mhe. Mjumbe ameuliza.

Ni kweli, imekuwa ikitokea katika baadhi ya nyakati, kuna baadhi ya viongozi wengine wamekuwa wakiwa na mkanganyiko katika suala hili. Lakini kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi. Serikali zetu zina utaratibu wa kufanya na ku-*resolve* mambo yake katika vikao vya mashirikiano baina ya serikali zetu zote mbili, baina ya SMT na ile SMZ. Kwa maana hiyo changamoto yoyote inayotokea kwa Waziri yeyote, iwe wa Zanzibar au wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, changamoto ile inapelekwa katika kikao kile na kikao kinajadili, kwa sababu kikao kinachukua Wajumbe wengi. Na kwa hatua za awali viongozi wetu Makamu wa Pili wa Rais na Waziri Mkuu wanahodhi kile kikao lakini *finalize* ya kikao kinakuwa *chaired* na Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa maana hiyo jambo lolote la kinidhamu ambalo mheshimiwa au kiongozi yeyote atakuwa amesema jambo ambalo halina afya na Muungano wetu pale ndio sehemu yake na maamuzi yote yanatoka katika kikao kile.

Nakushukuru Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Mheshimiwa naomba utaratibu.

Mhe. Spika: Mhe. Simai Mohammed Said naomba ukae chini.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nachukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Spika, tumekuwa tuna mambo ya Muungano na tuna mambo yaliyokuwa sio ya Muungano. Kuna zile wizara ambazo zinashughulika moja kuwa moja zimo katika Muungano na nyengine si za Muungano. Sasa tumekuwa tunashuhudia yale mambo ambayo si ya Muungano, Zanzibar inaposhiriki katika *International Arena* inayokwenda ni Jamhuri ya Muungano. Sasa kumekuwa kuna fursa na vitu vingi vinatolewa kwa mfano Wizara ya Kilimo, lakini vinatolewa kwa jina la Tanzania.

Sasa je, kuna utaratibu gani wa kuvipata vitu vile ambavyo vimetolewa kwa Tanzania lakini katika taasisi iliyokuwa si ya Muungano.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hassan Khamis Hafidh swali lake moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi. Wizara zetu zote za Muungano na zisizokuwa za Muungano bado zina fursa za kisekta za kushirikiana katika mambo yake, lakini hata katika msaada unaokuja ambao haupo katika mambo ya Muungano bado ule mgao wa Zanzibar unaendelea kubaki pale pale.

Lakini pia katika misaada ambayo Zanzibar imekuwa ikipokea kutoka katika mashirika na taasisi za kimataifa, bado misaada ile inapokuja kwa Jamhuri ya Muungano kunakuwa kuna mgao wake na bado sisi kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikipokea na ku-*receive* misaada mingi ya aina tofauti, ikiwa kwenye mashirika na taasisi mbali mbali kama ambavyo ushahidi umekuwa ukionesha. Hata Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alipowasilisha bajeti

yetu imeonesha kwamba bado tunayo mashirika ya kimataifa ambayo yamekuwa yakisaidia katika huduma nyingi. Kwa maana hiyo unapokuja msaada moja kwa moja kutoka kwenye taasisi ile Zanzibar tunaupokea kama tunavyopokea, tunashukuru tunapata ufadhili mkubwa katika sekta ya afya, tunapata ufadhili katika miradi ya maji, katika sekta za kilimo. Hiyo ni mifano katika maeneo ambayo tumekuwa tukipokea misaada ya namna hiyo.

Mhe. Spika nakushukuru.

Nam. 161

Uimarishaji wa Miundombinu Katika baadhi ya Masoko yaliopo katika Mji wa Chake Chake

Mhe. Simai Mohammed Said (Kny. Mhe. Suleiman Sarahan Said) – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uongozi wake Dr. Ali Mohamed Shein ameleta maendeleo mengi sana Zanzibar. Kwa kweli sifa zote zimwendee na mimi pia nampongeza sana kwa kuleta maendeleo zaidi hasa Mji wa Chake Chake umefaidika na ujenzi wa masoko yake mapya ya Kattar, Kuwait na naomba moja tulipate upande wa Chanjaani Chake Chake. Jambo la msingi sana, bado masoko hayo yanahitaji miundombimu na hasa soko la Kuwait ikiwemo eneo la kuteremkia magari naomba sana suala hilo litafutiwe ufumbuzi wa kitaalamu ili suala hilo lisijelikaleta maafa.

(a) Je, soko la Kuwait tayari mipaka yake inajulikakana na kuonekana dhahiri ili isijeleta migogoro baada ya wananchi kujenga ndani ya eneo hilo la soko.

(b) Kama mipaka hiyo ipo lakini pengine haionekani Je, Serikali haioni suala hilo ni muhimu na haraka sana lifanywe ili kuondoa utata wa baadae.

(c) Je, serikali ina mpango gani wa kuyagawa masoko hayo kwa hadhi na muonekano wake bila kuathiri Mji wa Chake Chake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 161 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba kwanza nichukue fursa hii kwa kusema Mhe. Mwakilishi alipokuwa anauliza swali lake alianza kwa pongezi juu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kubainisha kwamba juhudi ambazo zinazochukuliwa kubainisha kwamba ni kubwa na kuonesha pongezi. Kwa hivyo pongezi hizo na mimi niseme tumezipokea. Sasa nianze na jibu (a).

(a) Mhe. Spika, soko la Kuwait mipaka yake inajulikana na kwa heshima naomba nilijuilishe Baraza lako tukufu mipaka hiyo kama ifuatavyo;-

Kwa upande wa Kaskazini kuna kikuta ambacho kina nambari T269 na T270. Kwa upande wa Kusini kuna kikuta nambari. T273 na Kusini Magharibi kikuta nambari T274. Kwa upande wa Mashariki kuna kikuta ambacho kina nambari T271 na T272 na kwa upande wa Magharib kuna kikuta ambacho kina nambari T275.

(b) Mhe. Spika, vikuta hivyo viko wazi na vinaonekana. Hata hivyo, jitihada za kuweka alama maalum kulibainisha eneo hilo kwa uwazi zaidi zitafanyika.

(c) Mhe. Spika, kwa upande wa kuyagawa masoko yaliyomo ndani ya mji wa Chake Chake kwa hadhi na muonekano wake hili limo katika mpango maalum, ambapo soko la Kuwait tunatarajia liwe ndio soko kuu ambalo litakusanya bidhaa za aina zote. Soko la Qatar litakuwa ni soko la mboga mboga na samaki na masoko yaliyobaki yataendelea kama yalivyo. Mheshimiwa nakushukuru.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika ahsante, nikiendelea kuuliza swali la nyongeza kwa niaba ya Mhe. Suleiman Sarahan Said labda niulize.

Je, serikali ina mpango gani kuboresha masuala ya kuweza kuhifadhi vyakula kama nyama pamoja na samaki kwa ajili ya kujenga masuala kama ya *cooling system*, kama *cold rooms* ili wavuvi waweze kuhifadhi mali zao hasa kama samaki kwa muda ambao utakaoweza kuendeleza biashara zao kwa umakini zaidi. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako aomba nimjibu Mhe. Simai Mohammed Said, Mheshimiwa mahiri sana wa jimbo la Tunguu majibu kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Mheshimiwa kama nimemfahamu vizuri alitaka kujua na alitaka kwamba labda mkakati au mpango wa serikali kuhusiana na utaratibu ambao utaweza kusaidia wavuvi wetu katika masuala mazima ya kuhifadhi samaki katika mipango hiyo ambayo labda ametushauri.

Mimi niseme jambo hili kwa upande wetu sisi ni kwamba kwa kupitia miradi ambayo imeanzishwa, kwa mfano kama soko la Tumbe kule katika Wilaya ya Micheweni wamejenga soko kwa kweli liko imara na liko katika kuimarisha zaidi kulingana na vitu ambavyo amevishauri. Lakini kwa maeneo mengine naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba kama ushauri na kama mapendekezo nimuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba tutayachukua na nadhani vile vile kuna taasisi au kuna wizara ambayo inahusika moja kwa moja katika mambo haya Wizara ya Kilimo na Maliasili, lakini na sisi kwa upande wetu kwa sasa tunaelekea kwenye masuala mengine ya ugatuzi nadhani hayo ni mambo tutauchukua ushauri na tutayafanyika kazi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala dogo la nyongeza:-

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri wananchi wangu wa Ndagoni asilimia 80 ni wavuvi lakini wanapata tabu katika kuuza samaki kufuata masafa ya mbali Wesha. Je, ni lini wananchi wangu wale watajengewa soko la uhakika la kuuzia samaki na vitu vyengine aina kama hiyo ili kuondoka na usumbufu kule na kuacha na kuuza ile kienyeji na serikali kupata mapato yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR)Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niendelee kumjibu Mhe.Mwakilishi Mhe. Suleiman Makame Ali kutaka kujua kwamba ni lini wizara yetu ina mpango katika kusimamia kuona tunawasaidia wavuvi katika ujenzi wa masoko katika eneo la Shehia ya Ndagoni. Kwa kuwa ameonesha kwamba asilimia ya wavuvi ni kubwa.

Nataka niwambie Mhe. Mwakilishi kwamba juhudi kama hizi zinakuwa zikichukuliwa sana na taasisi yangu katika kuona kwamba kwa kupitia Mabaraza yetu ya Mji kuona kwamba tunaboresha hizo huduma na tunaondoa hizo kero za wananchi katika masuala haya ya upatikanaji wa soko. Lakini kwa sasa Mhe. Mwakilishi kwamba mji wa Chake Chake ni sehemu ambayo inaweza ikasaidia sana katika upelekaji wa huduma hata katika eneo jirani la

Ndagoni. Kwa maana hiyo, nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba avute subra kidogo tumalize hapa katika maeneo ya Mji wa Chake Chake, nadhani baadae tutaangalia uwezekano zaidi wa kuweza kusogea maeneo mengine kulingana na bajeti zetu ambazo tutakuwa nazo kupitia Mabaraza yetu na maeneo mengine.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuniona.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwanza napenda kuipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi mbali mbali ambazo inachukua kuwaondolea wananchi shida katika sekta tofauti.

Mhe. Spika, katika Jimbo langu Tumbe kuna soko kubwa ambalo lilijengwa kwa nia njema ya serikali ili wananchi pamoja na wavuvi wale wapate kutumia wasipate shida katika uuzaji wao wa samaki na uhifadhi wa samaki. Lakini hadi leo soko lile halitumiki.

Napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri. Je, wizara yake ina mpango gani wa kuhakikisha soko lile linatumika na wavuvi wale wanarudi kulitumia soko lile.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, naomba nichukuwe fursa hii kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe Mhe. Ali Khamis Bakari maarufu (Doholo) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli katika soko la Tumbe ni fedha nyingi za serikali zimetuka katika kuona kwamba inaondoa kero kwa wananchi wa maeneo ya pale na maeneo mengine katika kisiwa cha Pemba. Lakini la kusikitisha ni kwamba soko lile hadi sasa hivi wavuvi bado hawajalitumia kama vile Mhe. Mwakilishi ambavyo amesema.

Lakini mpango wa mkakati katika wizara yetu au katika taasisi yetu kupitia Mabaraza yetu na Halmshauri ya Wilaya ya Micheweni, juhudi mbali mbali zimekuwa zikifanyika kama taasisi tumekuwa tukifanya vikao mbali mbali kupitia na wizara nyengine. Kwa sababu jambo lile limekuwa likichanganya katika taasisi nyingi, hata wafadhili wake wametokana na maradi wa *MACEMP* ambao ni Wizara ya Kilimo. Kwa hivyo, tumekuwa tukifanya vikao mbali mbali vya kuona kwamba ni namna gani tunatengeneza mkakati wavuvi wetu waweze kurudi pale na lile soko liendelee kutumika ili kuweza kuleta tija.

Lakini kwa bahati mbaya sana hadi sasa hivi kupitia Halmashauri ni kwamba vikao kadhaa vimekaliwa katika kutengeneza mkakati kuona kwamba

tunafanya hivyo. Lakini lile jambo limeingia na mambo mengi yakiwemo mambo ya kisiasa. Hata hivyo nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi wizara yangu itafanya jitihada kwa kadri itakavyowezekana ione fedha zile za serikali zinatumika kama vile malengo yalivyokusudiwa.

Nam. 54

Kuanzishwa kwa Benki ya Wakulima

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza**:**

Kwa kutambua umuhimu mkubwa wa kilimo kua maendeleo ya Zanzibar na kwa kuzingatia hali ngumu za kiuchumi walizonazo wakulima wengi hapa nchini.

Kwa nini Serikali isianzishe kitengo cha Benki ya wakulima katika Benki ya Watu wa Zanzibar ili kuwanyanyua wakulima hao.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu Mhe. swali lake namba 54 la Mhe. Simai Mohamed Said kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa sekta ya kilimo imekuwa na mchango mkubwa katika uchumi na jamii yetu. Karibu theluthi moja ya pato letu la taifa linatokana na sekta hii ambayo pia imekuwa kimbilio kwa ajira kwa wananchi walio wengi. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali kusaidia wakulima, ikiwemo upatikanaji wa huduma za matrekta, usambazaji wa mbegu bora, mbolea na pembejeo kwa bei yenye ruzuku na kutoa huduma za ugani.

Juu ya kuanzishwa Kitengo cha Benki ya Wakulima, suala hili linahitaji wakati muafaka ili lisipelekee hasara kwa Benki yetu ya Watu wa Zanzibar ambayo kimsingi ni Benki ya Biashara. Kwa sasa huduma za *PBZ* hazibagui wateja kijinsia wala kisekta na kwamba sekta zote, ikiwemo Kilimo zina fursa ya kukopa.

Dhana ya kuwa na Benki ya Wakulima inahitaji mazingatio maalum ya sekta hiyo ambayo sio rahisi kuyafikia katika Benki ya Kibiashara kama vile ilivyo *PBZ*. Hata hivyo, wakulima hawajasahauliwa katika kupata huduma kwa Benki Maalum. Na tayari kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tayari kushaanzishwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo yenye Makao

Makuu yake Dar es Salaam, ambayo kimsingi imewalenga wakulima. Fursa iliyopo kwa benki hii zinapaswa kunufaisha pia wakulima waliopo Zanzibar.

Mhe. Spika, na ninaomba wito maalum kwa wakulima wetu wanaohitaji mikopo maalum wajitokeze kwa wingi na kuomba mikopo hiyo kupitia Benki hii ya maendeleo ya kilimo ilianzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo benki hii pia haifunguki kuanzisha tawi lake hapa Zanzibar. Na niseme tu kwamba tutachukua juhudi za kuwasiliana na wenzetu ili kuona uwezekano huo wa kuanzisha tawi lao hapa Zanzibar kama ilivyo kwa benki nyengine za kibiashara.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ambayo yenye ukweli na ufasaha kabisa.

Mhe. Spika, nilikuwa nina suala dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Zanzibar katika miaka ya 1980 na 1970 tulitegemea sana zao la karafuu katika pato letu la taifa na nchi ilijiendesha kwa kufaidika sana na wakulima wetu. Na ukiangalia kwa miaka ya leo bado kilimo kina nafasi kubwa katika wakulima wetu hasa katika visiwa vyetu ya Unguja na Pemba.

Je, serikali itafanya bidii gani kuhakikisha hii riba ambayo inapatikana katika Benki ya Watu wa Zanzibar ya asilimai 16, wanafanyiwa nafasi ya upendeleo ili serikali iweze kufidia na hatimae riba yake hii kuipunguza hadi asilimai 8. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said swali lake ya nyongeza kama ifuatavyo:

Kama nilivyosema kwenye jibu mama kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar ni Benki ya kibiashara na ina-*operate* katika mazingira ya kibiashara sambamba na benki nyengine za kibiashara. Na ndio maana tukasema kuitumia benki hii kwa kutoa mikopo kwa wakulima ambayo tunatarajia kwamba wakulima wetu watahitaji mikopo nafuu isingewezekana na si jambo la busara. Kwa sababu hivi sasa riba inayotozwa ni kati ya asilimia 17 hadi 18 na kwa mikopo mengine inakwenda hadi asilimia 19. Wale wanaochukua mikopo ya kutoka milioni moja hadi milioni 50 wanatozwa riba ya asilimia 19 na ukizingatia kilimo, *rate of return* ya kilimo ku-*investment* ni ndogo sana kufikia kuwa na uwezo wa kukopa katika kiwango hichi cha riba.

Mhe. Spika, sasa la kufanya, kwanza ni kuwahimiza wakulima wetu kulima kilimo chenye tija, wazalishe vizuri kwa kutumia teknolojia za kisasa. Lakini pia uhakika wa upatikanaji masoko ili kile kilimo kiwe na tija na kikiwa na tija hapo wanaweza sasa na wao kuingia katika mfumo wa kukopa kibiashara. Lazima kwanza kile kilimo chenyewe kiwe ni kilimo cha kibiashara kinazalishwa kwa tija, lakini vile vile wanapata masoko ya uhakika, wanapata kipato cha uhakika ili watakapokopa sasa wasibebeshwe mzigo, wawe na uwezo wa kurudisha mikopo hiyo.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi fursa ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye kutia moyo na yenye kufurahisha.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu Mkoa wa Kaskazini Unguja ni Mkoa ambao una wakulima pia wengi, lakini ukiacha wakulima una wavuvi wengi lakini pia una wafanyabiashara wengi. Lakini tukizingatia katika Mkoa huu wakulima hawa na wafanyabiashara hawa, lakini hata wale watu wa kawaida ambao wamejiunga katika hizi Benki za *PBZ* na nyenginezo bado wanapata shida kufuata mahitaji yao mjini.

Je, Mhe. Waziri kuna mpango gani wa kuwekewa japo *ATM* kusogezewa kwenye Mkoa wao ule angalau pale Kinyasini ili waweze kupunguza zile gharama za kufuata huduma hizi mjini kila muda, kila siku.

Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mhe. Hidaya Ali Makame kama ifuatavyo:-

Suala la kuwafikishia huduma za Kibenki wananchi ni suala ambalo liko katika mkakati wa Benki ya Watu wa Zanzibar, lakini lipo katika mkakati wa maendeleo ya kiuchumi ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hili ni suala ambalo halina mjadala na kama ilivyofanyika kwa kuanza kuweka hizi *ATM* katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Wazo lake la kuweka *ATM* katika eneo la Mkwajuni au la Kinyasini nalo litafikiriwa kwa kuzingatia vigezo ambavyo benki wenyewe wanavyo vya kuweka vituo hivi vya *ATM*. Kwa hivyo, hili wazo tunalichukua na wenyewe watu wa benki pale watakapohisi kuna haja ya kufanya hivyo, baada ya kukidhi vigezo ambavyo wameziweka basi *ATM* hiyo itakuwepo.

Lakini lengo kuu ni kusambaza huduma katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba ili wananchi wetu waweze kupata huduma za kibenki.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri na ya ufasaha ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri maswali yake kayajibu vizuri na kutoa wito kwa wananchi wetu kujua huduma za benki ni muhimu juu ya maisha yao. Lakini pia Mhe. Spika, nazipongeza benki zetu zote, lakini *PBZ* kwa kuwa imekusanya mambo mengi nawapongeza kwa kusaidia wananchi wetu hasa wanyonge. Swali langu lipo hapa.

Kwa kuwa Mheshimiwa suala la benki ni kitu ambacho kinamuwezesha mtu kupata mafanikio yake kwa haraka. Lakini bahati mbaya kuna taaluma ambayo inataka kutolewa juu ya kuwaelimisha wananchi wetu mbali mbali, hasa suala alilioliuliza Mhe. Hidaya Ali Makame kwa upande mmoja amenifilisi. Kuna wakulima na wavuvi naungana hapo hapo. Je, wizara inatoa wito gani kupitia Benki yetu ya *PBZ* ili kuwaelimisha wananchi wetu wakulima na wavuvi wajue kukitumia chombo hichi juu ya kupata faida katika maisha yao.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Suala la elimu ni suala muhimu na katika mipango yetu ya kuwawezesha wananchi wetu suala la taaluma hasa katika masuala ya kifedha ni jambo ambalo tunalipa kipaumbele sana. Katika kuwajengea uwezo wananchi ni lazima uwajengee uwezo kitaaluma lakini vile vile uwajengee uwezo katika masuala ya kutumia huduma za kifedha. Kwa hivyo, suala hili linatiliwa mkazo, benki inaendelea kutoa taaluma hizo, wana vipindi maalum ambavyo vinarushwa kupitia televisheni yetu *ZBC*.

Lakini vile vile kuna mkakati ya kukamilisha sera ambayo tunaita sera ya *Micro Finance*. Ndani ya sera hii kuna *component* maalum ya kutoa taaluma kwa wananchi wetu hasa wazalishaji wadogo wadogo katika sekta ya kilimo na sekta ya uvuvi. Sera hiyo iko katika hatua za mwisho kukamilika na baada ya kukamilika tutaanda mkakati maalum ambao utazingatia masuala ya kutoa taaluma kwa wananchi wetu kuhusiana na masuala ya kutumia huduma za kifedha hasa kupitia *Micro Finance Institution* lakini vile vile kupitia benki zetu za biashara zilioko nchini.

Nam. 151

Upatikanaji wa Sare za Wafanyakazi wa Shirika la Umeme Zanzibar

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza**:**

Mhe. Spika, kabla sijauliza naomba kidogo ufafanuzi. Bahati nzuri siku hizi tunapewa majibu kabla ya hata kuja kujibu swali pale. Lakini maswali yangu yana kipengele (a) na (b). Lakini jibu lililokuwa humu ni jibu la (a). Sasa jibu (b) sijapata ufafanuzi wake. Nitaomba sana mtu atakayekuja kunijibu swali langu, anijibu na kipengele changu cha (b). Kwa ruhusa yako naomba nipate jibu langu la swali namba 151.

Pamoja na jitihada nzuri za Shirika la Umeme kuendeleza na kuongeza ufanisi wa kuendeleza maswala ya miundombinu ya umeme katika nchi yetu ya Zanzibar, na kuwapendezesha wafanyakazi wa Shirika la Umeme kwa kuwapatia sare wafanyakazi hao.

(a) Je ni kigezo gani kilichochukuliwa cha kushonesha sare badala ya utaratibu wa zamani kuwapatia fedha wakashone wenyewe au kununua.

(b) Na ni gharama ya kiasi gani itachukua kugharimu ushonaji huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 151 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Utaratibu uliokuwa ukitumika hapo awali wa kuwapatia fedha za sare baadhi ya wafanyakazi haikuwa ni sharti la kisheria. Aidha utoaji wa fedha kwa wafanyakazi umepelekea kila mfanyakazi kuvaa mavazi yasiyoshabihiana kwa rangi na ubora na hivyo kuathiri taswira ya uvaaji wa sare katika Shirika.

Vile vile Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya 2011 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2014 zimeweka bayana kuwa ni wajibu wa muajiri kumpatia sare mfanyakazi. Hivyo uongozi wa Shirika unalazimika kufata utaratibu wa kisheria kama taasisi nyengine za serikali.

(b) Kwa sasa wizara yangu haitoweza kujua gharama za ushonaji wa sare hizo hadi mchakato wa zabuni utakapokamilika kwa mujibu wa taratibu za kisheria. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana pamoja na kupokea na swali (b).

Mhe. Spika, inashangaza anachoniambia kwamba Shirika lake au Wizara yake haitambui, wale wafanyakazi tayari wameshaanza kupimwa sare. Lakini ananiambia hajui thamani ya hiyo sare. Kwa hivyo naomba sana aniambie kwa sababu tayari nina watu tayari wameshaanza kupimwa sare. Sasa swalia langu.

Mhe. Spika, tayari wameshaanza kupimwa sare lakini Mhe. Naibu Waziri anasema kwamba huwezi kujua kwa sababu thamani hujaijua. Hapo haiingii akilini kwangu mimi. Ni kampuni gani iliyoshinda tenda ile mpaka kufikia watu wale kuanza kupimwa sare na tenda hiyo imepita kwenye taratibu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Diwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kwamba zabuni zinategemewa zifunguliwe tarehe 16 mwezi huu. Kwa hivyo kampuni gani, tutajua baada ya kushinda. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Tunaendelea. Swali linalofuata.

Mhe. Mjumbe hujaridhika na majibu au vipi. Sawa basi tunakuomba Waziri yupo hapa unaweza ukasogea ukazungumza naye. Sisi tuwache tuendelee.

Naomba ukae Mheshimiwa. Tunaendelea.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Naomba ukae. Tunaendelea. Spika anaweza akakataa utaratibu. Nimeukataa utaratibu wako Mhe. Mjumbe.

Swali linalofuata ni la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, swali linaulizwa na Mhe. Swaib Said Ali Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chonga.

Nam. 34

Umiliki wa Eka 10 Kwa Kila Skuli za Unguja na Pemba

Mhe. Shaib Said Ali – Aliuliza:-

Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, aliipatia kila skuli za Unguja na Pemba eka 10 kwa lengo la kuondoa uvamizi wa kujenga, kufuga au kuchunga wanyama karibu na maeneo hayo.

(a) Je, ni skuli ngapi za Unguja na Pemba zinazoendelea kumiliki eka hizo hadi leo.

(b) Je, zile ambazo hazimiliki tena eka hizo, ni sababu gani zilizopelekea kunyang'anywa ardhi hizo.

(c) Kuna utaratibu gani wa zile skuli zilizonyang'anywa eka hizo kurudishiwa ardhi zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 34 lenye sehemu (a), (b), na (c). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Mhe. Marehemu Aboud Jumbe Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili wa Zanzibar, aliagiza skuli zilizokuwepo wakati huo zipatiwe eneo la ekari kumi kwa kila skuli, kwa madhumuni ya kuendeleza kilimo katika skuli zetu ukiwa ni utii wa mgongo wa uchumi wetu.

Baadhi ya skuli zilipatiwa maeneo hayo na yalitumika katika kuendeleza kilimo katika skuli. Baadhi ya vyuo na skuli hizo ni kama vile Chuo cha Ualimu Nkrumah, skuli ya Bambi, Mwera, Kiboje, Donge, Umbuji, Bambi, Uzini, Uroa, Chwaka, Charawe na Mkwajuni kwa upande wa Unguja na baadhi ya skuli hizo kwa kwa Pemba ni Skuli ya Sekondari ya Fidel Castro, Kinyasini, Mchangamdogo, Kangagani, Minungwini, Shengejuu, Pandani, Piki, Mitiulaya, Gando, Ukunjwi, Kizimbani, Makongeni, Kinyasini, Tumbe, Shumba Msingi, Wingwi, Chambani, Kiwani, Chokocho, Ukutini, Uweleni, Kilindi, Ole, Birikau kwa kutaja baadhi.

Maeneo hayo makubwa yalipimwa na skuli kupatiwa hati miliki. Hata hivyo, maeneo mengi yalikuwa ni ya wazi na hayakuzungushwa uzio kwa ajili ya kuyalinda.

Baada ya maelezo hayo, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, hivi sasa wizara haina idadi kamili ya skuli zetu zinazoendelea kumiliki eka zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo.

(b) Mhe. Spika, matumizi ya baadhi ya maeneo hayo yamebadilika, katika baadhi ya skuli kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi, maeneo hayo yametumika kwa ujenzi ama wa skuli mpya au Taasisi za Elimu nyengine, na maeneo mengine yamevamiwa na kutumiwa kwa ujenzi wa makaazi ya watu.

Kwa Mfano, Chuo cha Ualimu cha Nkrumah kilikuwa na eneo la kilimo huko Mkokotoni ambalo sehemu ya eneo hilo hivi sasa limejengwa Kituo cha Mafunzo ya Amali. Pia, ekari za skuli ya Donge zimetumika kwa ujenzi wa skuli ya Maandalizi, skuli mpya ya sekondari, Kituo cha Afya na Msikiti na eneo lilobakia linaendelezwa kutumiwa kwa shughuli za kilimo cha skuli.

(c) Mhe. Spika, wizara yangu kwa ushirikiano na Wizara inayohusika na masuala ya Ardhi, inaendelea kuyapima maeneo yote ya skuli zote ambayo hazina hatimiliki za maeneo yao na hatimaye kupatiwa hatimiliki. Hii itapelekea skuli zote kuweza kujua na kudhibiti ukubwa wa maeneo yao. Kwa skuli ambazo maeneo yao yamenyang'anywa au yamevamiwa, taratibu za kisheria zitafuatwa kuhakikisha ufumbuzi unapatikana. Ahsante.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, lakini Mhe. Spika, nina swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba bado kuna skuli ambazo zinaelezea kwamba hawazijui skuli ambazo zinamiliki maeneo yao. Je, wana mpango gani wa kuyatambua maeneo hayo ili kuondosha usumbufu huo.

b) Ni lini basi watayapima maeneo hayo yaliyobakia na kuwapatia hati miliki ili kuondosha usumbufu ambao jamii sasa hivi inazivamia skuli hizo

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Shaib Said swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

a) Ni kwamba imekuwa ni vigumu kuyatambua kwa sababu kama tulivyoeleza, baadhi ya skuli maeneo hayo yamechukuliwa robo, baadhi nusu, baadhi yote na kadhalika. Lakini hata hivyo sasa hivi tunaendelea kuyafuatilia ili kujua kiasi gani kilichochukuliwa kwa kila skuli na kimetumika kwa madhumuni gani. Zoezi hilo tutalifanya wakati wowote kuanzia sasa.

b) Kuhusu lini yatapimwa. Swali hili tumelijibu mara nyingi na tunarejea kwamba sasa hivi kwa kushirikiana na Wizara inayohusika na Ardhi, utaratibu umewekwa wa kuyapima maeneo yote ya skuli na kwa sasa tutaanzia na Wilaya ya Magharibi.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alisema katika jibu lake mama kwamba kuna baadhi ya maeneo yamevamiwa na wananchi. Kama wananchi wamevamia maeneo hayo na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunaamini kwamba baadhi ya nyakati mnakwenda kukagua katika zile skuli.

Je, hamuoni kwamba hamtawatendea haki wananchi wale ambao wameshajenga majengo yao ya kudumu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Bahati Khamis swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Tumesema kwamba baadhi ya maeneo haya yamevamiwa na tukasema kwamba taratibu za kisheria zitafuatwa ili kuweza kulitatua tatizo hili. Lakini pamoja na kutumia taratibu za kisheria, lakini busara, hekma na ubinadamu utatumika.

Mhe. Mwanaid Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alituambia kwamba wana mashirikiano mazuri baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, wamesema tayari wanataka kupima maeneo ya maskuli. Mimi nataka nijuwe wameanza katika Wilaya ya Magharibi.

Je, katika Wilaya ya Magharibi ni skuli ngapi tayari zimeshaanza kupimwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwanaidi Khamis Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kwamba katika mazungumzo yetu na mashirikiano yetu na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira tulisema kwamba skuli zote zipimwe na zipatiwe hati miliki. Lakini katika vikao ambavyo tumekaa nao vya watendaji, tulisema kwamba tuanze na Wilaya moja na tukaamua kwamba tutaanza na Wilaya ya Magharibi.

Sasa hivi tunakwenda katika hatua ya kukamilisha taratibu za kifedha za kuweza kupima, na wakati ambapo zoezi hilo litaanza basi tutaona hali yenyewe itakavyokuwa. Lakini sasa hivi halijaanza isipokuwa kuna taratibu za kifedha ambazo tunazifanya.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niongezee jibu zuri zuri ambalo amelijibu Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba kwa mashirikiano makubwa Wilaya ya Magharibi "A" tumeanza kupima na karibu skuli zote zimeshafanyiwa *PG* na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wamelipa na kazi inaendelea.

Kwa hivyo, naomba kutoa taarifa Baraza lako tukufu waweze kujua na wananchi kwa jumla.

Nam. 23

Tatizo la Kituo cha Afya cha Kiuyu – Minungwini

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi inastahiki pongezi kwa kuhakikisha kuwa wananchi wake wanapata huduma ya afya kwa kujenga vituo vya Afya katika vijiji vingi nchini. Hata hivyo, kuna changamoto ambayo inawakabili wananchi wa Kiuyu – Minungwini tokea walipokihama kituo chao cha Afya kutokana na ubovu wa

jengo hilo na Wizara kutoa ruhusa ya kuhama na kwenda kuhamia katika jengo la mtu binafsi.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kukijenga kituo kile.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:-

Nashukuru Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia sote tukiwa hapa leo wenye afya njema na wazima na kutimiza majukumu yetu katika kuwatumikia wanachi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi mahiri anayewawakilisha wanawake swali lake Nam. 23 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijamjibu kwanza tunamshukuru sana Mhe. Viwe Khamis, kwani yeye pia ni Mjumbe wetu wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, lakini pia tunamshukuru kwa pongezi zake kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia na sisi tutahakikisha kwamba pongezi hizo zinafika kwa kiongozi wetu ambaye anasimamia sekta hii ya afya kwa umahiri, kwa hekma na busara kubwa na yeye sio mwengine bali ni Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na hususan kwa hatua kubwa ambazo zimekuwa zikichukuliwa hivi karibuni katika sekta ya afya kwa miongozo yake na maagizo yake, ambapo tayari vituo kadhaa vimeshaanza kujengwa kwa agizo lake moja kwa moja, kikiwemo kituo cha Ngomeni kwa kule Pemba kipya kabisa na kituo cha Mgonjoni kilichopo Wilaya ya Kati kwa hapa Unguja. (*Makofi*).

Mhe. Spika, sasa naomba nimjibu Mhe. Viwe Khamis Abdalla kwamba ni kweli wanachi wa Kiuyu Minungwini wanakabiliwa na changamoto kubwa kidogo ya Kituo chao cha Afya, baada ya kituo kilichopo kuhamwa kutokana na ubovu wa kituo hicho. Wizara yangu tayari inalielewa suala hilo na Mhe. Naibu Waziri ameshalitembelea na hivi sasa tayari imeshaanza kuchukua hatua ya kupima eneo lililokuwepo karibu na kituo hicho, pamoja na kuomba hati ya kumiliki ardhi baada ya kupima eneo hilo, jambo ambalo tayari limeshafanyika na hatua husika zimefikia pahala pazuri sana.

Aidha, wizara yangu imefanya mazungumzo pia na wafadhili mbali mbali kwa ajili ya kujenga kituo hicho, tukishirikiana na bajeti yetu moja kwa moja kwa kupitia Wizara ya Afya. Kwa hivyo, naamini baada ya kipindi cha bajeti na kumaliza vituo hivi vya Ngomeni na Mgonjoni, basi tutaelekea huko moja kwa moja Kiuyu Minungwini. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanaleta imani kwenye nafsi yangu na moyo wangu ya utekelezaji wao katika kituo hiki.

Mhe. Spika, kwa kuwa kituo hiki tayari kimeshachukua muda mrefu na bado utekelezaji wake haujaonekana. Je, ni lini mpango huu utakamilika na kuanza utekelezaji wake.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Viwe Khamis Abdalla swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, nasita kutoa tarehe ama mwezi ni lini, kwa sababu hivi sasa vituo hivi viwili tulivyokuwa navyo tunavijenga ambapo kimoja kilipata bahati hivi karibuni kutembelewa pia na Mhe. Rais tulivyokuwa naye kwenye ziara kule Pemba Ngomeni na kutoa maagizo mbali mbali ya kufanya marekebisho katika kituo hicho. Nasita kusema ni lini, kwa sababu mpaka hivi vituo viwili vimalizike ndio tutaweza kutoa nguvu zetu tuelekee Kiuyu.

Kwa hivyo, mimi namuahidi Mhe. Viwe Khamis tutakwenda pamoja kule Kiuyu na mimi mwenyewe nitakwenda naye pamoja tutafuatana. Yeye ajitayarishe tu kutupokea vizuri na kutukaribisha kule, lakini tutakuwa pamoja pale wakati wa ujenzi tukianza.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei): Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Lakini kwanza nianze na pongezi kwa Mhe. Waziri ambaye kwa kweli ni msikivu na ni mtenda kazi pale anaposhauriwa.

Mhe. Waziri kwa kuwa ni hodari wa kutatua changamoto za Wizara ya Afya, Hospitali ya Vitongoji sasa hivi zaidi ya miezi mitatu gari la wagonjwa halifanyi kazi pale na tatizo ni kitu kidogo sana, ni mvutano wa uongozi wa hospitali na mafundi wa wizara. Lakini nashukuru wizara imetoa pesa za matengenezo ya gari zile.

(a) Je, ni lini utakwenda Pemba kuondoa tatizo hili ili wananchi wetu wa majimbo ya Wawi na Ole na majimbo jirani waweze kupata huduma ya gari hilo.

(b) Kwa sababu hospitali ya Chake Chake kuna magari mawili ya wagonjwa. Huoni kwamba kuna haja ya kuomba gari moja la Chake Chake litumike Vitongoji hadi hapo lile litakapokuwa tayari.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba arudie swali (b) sikulisikia kabisa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe swali (b) halijasikika vizuri naomba ulirudie.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei): Mhe. Spika, kwa sababu Hospitali ya Chake Chake kuna magari mawili ya kuwabebea wagonjwa na yote ni mazima. Huoni kwamba kuna haja sasa lile gari moja kuazimwa Hospitali ya Vitongoji ili likaweza kutoa huduma kwa wananchi wetu wanyonge ambao wanapata tabu na kudhalilika kukosa huduma ya usafiri.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hamad Abdalla Rashid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, kwanza namshukuru na yeye pia kwa mashirikiano anayotupa ya karibu sana pale ambapo Mwakilishi wa wananchi akiwa na tatizo moja kwa moja. Kwa sababu Wwawakilishi wa wananchi wanakuwa karibu na wananchi zaidi, kwa hivyo wakati mwengine matatizo wao huyapata mwanzo hata kuliko uongozi wa juu wa wizara. Nashukuru alipoliwasilisha hili suala la *Ambulance* katika Hospitali ya Vitongoji, tayari tumeshafanya mawasiliano na Afisa Mdhamini na tayari limetatuliwa na wale waliokuwa wanafanya mambo ya kuvutanavutana kidogo wameshapewa onyo la mdomo kwanza. Kwa hivyo, hilo tayari limeshatatuliwa na hivi sasa Afisa Mdhamini analisimamia. Nashukuru sana.

(b) Kuhusu magari yale mawili yaliyokuwepo pale Hospitali ya Chake Chake, naomba yale magari yaendelee kubakia pale, kwa sababu Chake Chake ina *volume* kubwa ya wagonjwa, yaani nikisema *volume* ni wingi wa wagonjwa hata kuliko Hospitali ya Abdalla Mzee sasa hivi, wengi wanakwenda Chake Chake kwa sababu ndio mjini na wanaotokea Kaskazini kule wote wanafikia pale Chake Chake. Magari yale naomba yabakie pale ila tumepewa hivi karibuni msaada wa magari ya *Ambulance* tunazo karibu gari nne mpya na Shirika la *UNFPA* la ulimwengu ambao wametupa magari manne. Magari mawili tunatarajia kupeleka Pemba na moja tutapeleka katika Hospitali ya Vitongoji. Kwa hivyo, tunaomba mtuvumilie tu tunakamilisha taratibu za kupeleka. Nnashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu mazuri katika wizara yake. Lakini katika swali la msingi imebainika kuonekana kwamba Kituo cha Afya kilihamishwa kikahamia katika jengo la kukodi.

(a) Je, Mhe. Waziri huyu mmiliki wa hili jengo alilitoa kwa wizara yako bila ya malipo yoyote.

(b) Kama wizara iliingia mkataba. Je, ni utaratibu gani wa kumpata mkodishaji ambaye wizara iliingia naye mkataba na kiasi gani cha fedha kilitumika. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza) swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa taarifa nilizokuwa nazo mimi na kwa ninavyoelewa huyu mwananchi amejitolea, ameona kuna tatizo pale ni mwananchi mwema wa nchi hii, mwenye kupenda maendeleo na mwenye kuiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, amesema ana jengo pale jirani ambalo halitumiki, kwa hivyo amejitolea amesema mnaweza kulitumia jengo hili mpaka pale sisi tutakapokuwa tayari.

Mhe. Spika, jengo lile ametupa bila ya masharti yoyote mpaka hivi sasa. Tulichokifanya sisi na sisi pia hatukumpa masharti yoyote, ila wale *staffs* wetu waliokuwepo pale Kiuyu Minungwini ndio wameingia kwenye jengo hili ambalo yeye mwananchi ametuazima, tulilifanyia kidogo marekebisho ili kufanana na huduma ambazo tunazotoa pale na tunaendelea kutoa huduma bila ya masharti yoyote kwa huyu.

Kwa hivyo hajatukodisha wala hajatupa masharti yoyote ni mwananchi mwema ambaye amejitolea. Lazima mimi nimpongeze kwa moyo huo wa kujitolea kwa sababu hivi ndivyo tunavyotakiwa tuwe. Sadaka ziko za aina nyingi na katika sekta ya afya ndio sadaka yenyewe huko. Kwa hivyo naamini na Mwenyezi Mungu atamlipa kwa wema wake huu alioufanya. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Kuna swali moja la nyongeza la upendeleo Mhe. Mwanaasha na alisimama sana alionekana alikuwa na kitu.

Mhe: Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana, Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya upendeleo hasa ukizingatia ajenda ni mwanamke.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya ambaye pia ni Mwakilishi wangu wa Jimbo la Kiembe Samaki, naomba kumuuliza swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Kwa kuwa Wizara yake imeanzisha vituo mbali mbali za afya katika maeneo tofauti kuwaondoshea wananchi usumbufu katika maeneo yao na kuondosha msongamano mkubwa katika Hospitali Kuu hasa ya Mnazi Mmoja.

a) Je, Wizara yake ina mpango gani katika kuzifanyia ukarabati vituo vya afya chakavu hasa kituo kilichopo Shakani katika Jimbo la Chukwani.

b) Hii ikiwa kituo cha Afya cha Shakani ni miongoni mwa vituo vilivyochakaa, ni lini kituo hicho cha afya kitafanyiwa ukarabati.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako kumjibu swali la nyongeza lenye upendeleo maalum, Mhe. Mwanaasha Mwakilishi wangu pia wa Jimbo la Chukwani ndiko ninakoishi lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwanza kabisa naomba aondoshe hofu na mashaka, katika mwaka huu tutakaposoma bajeti yetu tutakuwa na *target* ya kuvifanyia ukarabati jumla ya vituo 38, hiyo ni bajeti yetu serikali Wizara ya Afya ikishirikiana na ndugu zetu wa *Milele Foundation* na *project* ya tatu ni wale Waholanzi waliojenga majengo mawili pale Mnazi Mmoja. Wao pia nao tutashirikiana nao kuna mradi ambao uko kwenye hatua za mwisho sasa hivi wanafanya *logistic* za kuweza kuanza.

b) Wao kwa upande wao fedha zao zichakamilika tayari kwa sababu wao wanapewa nusu, na sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunatoa nusu. Kwa hivyo vituo 38 vitafanyiwa ukarabati. Hapa sina uhakika kama Shakani kipo ama hakipo ila nitakwenda kutazama halafu niweze kumpa majibu Mhe. Mwanaasha ambaye tuko naye karibu sana kimawasiliano.

Jengine nnataka kusema kwamba vituo vile ambavyo hali yake itaonekana, kuwa si nzuri basi mbali ya hivyo vituo 38 ambayo orodha yake nitaiwasilisha pia katika *budget speech* yetu ya Wizara ya Afya ili kila Mwakilishi aweze kujua, kituo kipi kilichomkusa katika jimbo lake ama katika eneo lake la Uwakilishi wake maalum analowakilisha humu ndani ya Baraza.

Kwa hivyo vituo vitakavyoonekana bado vinahitaji ziada ya ukarabati, basi navyo tutaviingiza katika orodha hiyo tunashukuru ufadhili katika eneo hilo bado tunao, na tutaendelea kushirikiana na Wawakilishi pale wanaporipoti kwamba pana ukarabati mkubwa utakaohitajika katika eneo hilo.

Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 103

Majanga ya Kuporomoka Nyumba za Mji Mkongwe

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:

Hivi karibuni kumekuwa na majanga ya kuporomoka nyumba za Mji Mkongwe na kusababisha vifo, majeruhi na vilema. Kwa vile imeonekana kuwa majengo mengi ya eneo hilo yamechakaa na yanahitajika kufanyiwa matengenezo na Serikali imeshindwa kuyafanyia matengenezo hayo.

(a) Je, kuna tathmini yoyote imefanyika kubaini idadi ya majengo ambayo hayawezi kutumika na yatahitaji kufanyiwa matengenezo na idadi gani ya majengo ambayo ni mazima.

(b) Kuna mpango wowote wa kufanya matengenezo kwa majengo yaliyo kwenye hatari ya kuporomoka.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika**,** Ahsante sana kwa kunikaribisha katika Baraza lako Tukufu ili kujibu maswali lakini kabla sijaendelea na kujibu maswali nilikuwa nataka nimuombe Mwenyezi Mungu atujaalie kheri na kumshukuru kwamba leo tumekutana hapa afya nzuri na niko tayari sasa kujibu yale maswali. *(Makofi)*

Mhe. Spika**,** kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, katika Kikao cha Baraza la Mapinduzi kilichofanyika tarehe 28 Disemba, 2016 Serikali iliiagiza Wizara yetu kufanya tathmini ya majengo ya Serikali yaliyoko katika Mji Mkongwe wa Zanzibar, na lengo la tathmini hiyo ni kubaini idadi na hali ya mahitaji ya matengenezo ya nyumba hizo na kuwasilisha gharama za matengenezo hayo.

b) Mhe. Spika, Shirika la Nyumba la Zanzibar kwa kushirikiana na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe ilifanya tathmini hiyo na kubainisha jumla ya nyumba 26 katika Mji Mkongwe wa Zanzibar ambazo zinahitaji matengenezo makubwa. Gharama kwa jumla za matengenezo hayo ni shilingi bilioni 11,778,118,075.

Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika pamoja na majibu ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza;-

Kwanza nimpongoze Mhe. Waziri kwa kuangalia uhai wa watu wetu wanaoishi katika majumba hayo, na ndio maana Baraza la Mapinduzi likakaa na kufanya tathmini juu ya athari ambazo hatutegemei zitokee kama mafuriko ya mvua yaliyotukuta katika maeneo ya bondeni. Swali langu lipo hapa.

Je, Mhe. Waziri kwa kuwa wananchi wetu wengi wanaishi katika majumba hayo mabovu ambayo yamefanyiwa tathmini na bado wanaendelea kuishi na mvua hizi zinaendelea. Serikali ina wito gani kwa wananchi wao kuondoka ili waondokane na maafa ambayo Mwenyezi Mungu asiyalete katika maeneo hayo kuhatarisha afya zao na maisha yao ya baadae. Ina maandalizi gani ya kuwaondoa hao wananchi wanaoishi katika majumba 26 kwa kuwa mvua zinaendelea ni hatari kwa maisha yao. Serikali ina mpango gani kuwaondoa watu hao hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwenye swali hili la mvua ningependa kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba mvua hii ina faida kwa watu wengine na upande mwengine kuna madhara.

Lakini ukiangalia kwamba sisi tunategemea zao la karafuu. Na karafuu wenyewe wataalamu inahitaji mvua nyingi. Sasa kwa upande huo wao wanaomba mvua iwe nyingi ili karafuu ziwe nyingi, lakini mvua hizo hizo zinavuruga njia zetu kule Pemba, mvua hizo hizo zinaleta matatizo mengine lakini kwa upande huu nataka Mhe. Mwakilishi ujue kwamba hizo mvua hizo ambazo zinatuharibia kwa upande tunaziomba pia zitusaidie katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Sasa nikijibu swali lako Mhe. Mwakilishi, nasema masuala ya Mji Mkongwe na matatizo ambayo tunayo ya Mji Mkongwe, ni matatizo ambayo yanatokea dunia nzima na yanatokea kwa sababu gani, kuna kitu kinaitwa *Urban DK*,

yaani miji iliyojengwa zamani, halafu ikawa utunzaji wa yale majengo si mzuri, inafika wakati sasa hata ukitaka kuyatengeneza gharama zake zinakuwa ni kubwa zaidi kuliko kujenga nyumba mpya.

Sasa katika hizi nyumba 26 zilizoonekana zinaonekana kwamba hizi kwa kisheria na sheria tunatunga wenyewe hapa, kwa kisheria nyumba hizi ziwe *condemn* na zishakuwa *condemn* wale watu wanaoishi kule ndani wahamishwe. Lakini mara nyingi watu wetu tunawajua ni ndugu zetu, dada zetu, ndio binamu zetu, ndio rafiki zetu, ukiwambia wahame hawataki kuhama. Kwa kuwa wizara hii ndio inashughulika pia mambo ya ujenzi na Shirika la Nyumba liko huku, wananambia kabisa hasa Waziri wewe unapo pa kukaa, sisi tuhame hapa tunahamia wapi. *(Makofi)*

Sasa siku nitakapoulizwa swali hilo nitakukaribisha na wewe Mheshimiwa uje pale tupate majibu ya kuwajibu hawa. Kwa hivyo kwa ufupi nasema wanakataa kuhama. Kwa hivyo hilo tukae tuchange mawazo hapa, pengine itabidi tuunde sheria hapa ya kuwahamisha wale watu kwa nguvu. Lakini Naibu Waziri wangu yeye ndio Mwakilishi wa Mji Mkongwe, nilipowahi kumnong'oneza kuhusu hilo akaniambia aah! hilo tulifikirie tena kwa sababu yeye ana watu wake kule waliompigia kura kule. Kwa hivyo kwenye hilo natumai kwamba jibu langu limetosheleza.

Ahsante Mhe. Spika *(Makofi)*

Mhe. Spika: Yametosheleza Mheshimiwa, tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini kwenye wizara hiyo hiyo.

Nam. 146

Ukiukaji wa Taratibu za Uhifadhi wa Mji Mkongwe

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini - Aliuliza:

Hoteli ya *Lukuman* iliyopo Kiponda imevunja utaratibu wa mzunguko wa magari na *parking* uliokuwepo hapo zamani mbele ya jengo lao kufanya hoteli na wametengeneza msitu bandia wenyewe wanaouita bustani.

(a) Je, Wizara yako kwa nini imeliruhusu jambo hilo kutendeka kinyume na taratibu.

(b) Mamlaka ya Mji Mkongwe haioni kama inavunja utaratibu wa Uhifadhi wa Mji Mkongwe inayoweza kuleta sifa mbaya na kupelekea kupewa hati chafu na *UNESCO*.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ufupi nikependa kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba Shirika la Nyumba la Zanzibar ninaandaa mpango wa matengenezo wa nyumba hizi sambamba na matengenezo ya nyumba zake nyengine katika mpango huu ambao utakuwa na awamu tatu:

Awamu ya kwanza ni matengenezo ya haraka. Awamu hii inajumuisha nyumba 26 zile ambao ziliulizwa katika hali mbaya na gharama za awamu hii ni kama zilivyotajwa awali bilioni 11.

Awamu ya pili ni mpango wa matengenezo wa muda wa kati. Awamu hii inajumuisha jumla ya nyumba 7 na itahitajia shilingi milioni 72.

Awamu ya tatu ni mpango wa muda mrefu. Awamu hii inajumlisha jumla ya nyumba 44 na inahitaji jumla ya shilingi milioni 16.

Mpango huo pia, umebainisha jumla ya nyumba 11 ambazo zinaweza kukodishwa kwa wawekezaji kwa mikataba ya muda mrefu. nyumba zilizobainishwa zina gharama ya matengenezo ya shilingi milioni 7.

Mhe. Spika, nikija sasa katika kujibu swali la Mhe. Mwakilishi nataka kusema tu kwamba kwa ruhusa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yetu haijamruhusu mwenye hoteli ya *Lukman* kufanya bustani ya bandia, isipokuwa mmiliki wa hoteli hiyo aliomba kuliimarisha eneo hilo kutokana na hali mbaya iliyokuwepo hapo awali. Aidha, Mamlaka ilimruhusu mhusika kutengeneza eneo hilo kwa kufuata maelekezo aliyopewa ambayo yalizingatia uasilia wa eneo hilo. Katika eneo hilo hapakuwa na ruhusa ya matumizi ya *parking*.

(b) Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba Mamlaka ya Mji Mkongwe haivunji utaratibu wa Uhifadhi wa Mji Mkongwe, na inajitahidi kuhakikisha kwamba Kanuni na taratibu za utunzaji na uhifadhi wa Mji huo zinatekelezwa. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, nataka niongeze kidogo kwenye majibu haya kwamba kihistoria kuna wakati

tuliulizwa maswali mengi sana na watu wa *UNESCO* wameshughulikia wanaitwa *World Heritage Site.*

Kwamba kwa nini tulikwenda tukavunja sheria ambazo zimewekwa na hizi ni Sheria za Kimataifa. Na nimezungumza na Mwanasheria Mkuu akaniambia ndio Sheria za Kimataifa lazima tuzifuate. Tuna sheria zetu hapa na Sheria za Kimataifa tunazozifuata na hizo Sheria za Kimataifa tunazotiliana mkataba, hatutii mkataba mpaka kwanza tuje katika Baraza la Wawakilishi tumfanye *ratification,* yaani mkubali tuingie katika huo mkataba.

Kwa hivyo tukiingia katika mkataba huo wa *World Heritage Site*, una faida na sisi na tuulizana tubaki huko au tutoke. Maana ziko nchi nyengine miji imetolewa. Mfano Muscat kule Oman wameona kwamba Sheria zile ni ngumu zinawazuwia kufanya shughuli zao wanavyotaka. Wakenda kule kasema tutoweni, wakatoka. Sisi tumefanya uamuzi wa Kiserikali kwamba tunabaki huko na sababu zake zipo, hasa mambo ya utalii na pia kuhakikisha kuwa zile nyumba ambazo zilizojengwa zamani tunazihifadhi ili na watoto wetu na wajukuu wetu waje wazione. *(Makofi)*

Sote hapa Wazanzibari tunakumbuka siku ya kwanza tulipokwenda kuliona Beit-el Ajaib. Na hiyo Beit-el-Ajaib inaitwa hivyo kwa sababu wengi walikuwa wanasema ni nyumba ya ajabu. Kwa hivyo mimi nasema Ng'ome kongwe, nyumba ya ajabu na majengo mengine yoyote yaliyojengwa zamani tuyahifadhi.

Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi ningependa kukuhakikishia kwamba tumezifuata Sheria hizo tunafuata Kanuni na kwamba iliwahi kutokezea tukahatarishwa kufukuzwa, wakati mpaka hoteli ya *Hayatt* ilipokuwa inatengenezwa, wakenda kinyume na utaratibu uliowekwa. Tukaitwa tukaambiwa kama hamtofanya marekebisho mtafukuzwa.

Mhe. Spika, na nakumbuka kwamba haya yote yalipofanyika, yalifanyika kutokana na uongozi dhaifu na usimamizi mbovu na inasikitisha kuona kwamba kwa wakati huo Mhe. Mwakilishi wewe ulikuwa umekamata nafasi kubwa sana ya Uwaziri katika nchi yetu.

Napenda kukuhakikishia kwamba makosa kama hayo hayatotokea tena. *(Makofi).*

Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa yeye kama ni *carrier diplomat*, ameonesha kweli busara za kutanzua matatizo ya Mji Mkongwe. Ninakupongeza sana.(*Makofi*).

Sasa naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza naomba tena nimshukuru kwa kukiri kuwepo hili tatizo na kwamba huyu mwekezaji pale hakuruhusiwa, lakini amefanya tu kwa utashi wake. Sasa baada ya kukiri tatizo hilo Mheshimiwa kama nilivyosema wewe ni mwana falsafa na busara zaidi unaitanguliza. Wizara yako imejipanga vipi na lini kuihamisha bustani ile ili wananchi hao uliowazungumza wa Mji Mkongwe tusiwa-*disturb*, tusiwape bughudha ili wapite vizuri katika lile eneo. Maana ile bustani imeziba ule mzunguko wa ile sehemu. Lini Mheshimiwa na busara zako utalitanzua hili tatizo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ningependa kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba hili tatizo tunaweza tukasema ni tatizo ambao ni *debatable*. *Debatable* maana yake kuna wengine wanasema kilichofanyika ni halali, kuna wengine wanasema hapana, kuwa kilichofanyika si halali.

Sasa hiyo ni kazi yangu mimi kama Waziri muhusika kwenda kulifuatilia na Mamlaka nitawaita tukae kitako tuangalie, zamani pale palikuwa vipi na sasa huyu kafanya nini. Kwa kweli hapo zamani walikuwa hawaruhusu *parking*. *Parking* walikuwa hawaruhusu *parking* magari kama yalikuwa yanapita lakini sasa hivi hayawezi kupita. Hilo tatizo lazima lirekebishwe. Kwa hivyo nakuhakikishia kwamba hili nitalifuatilia na nitakapopata fursa nyengine ya kujibu maswali kama haya nitakuja kukwambia hatua ambazo zimechukuliwa. (*Makofi*).

Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Makame Shamshi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kulipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mhe. Waziri anayehusika na Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, lakini kabla ya hapo nimshukuru na nimpongeze sana kwa ufasaha na ufafanuzi mkubwa wa swali mama pamoja na lile swali la nyongeza la Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini.

Mhe. Spika, katika kumbukumbu zangu kupitia vyombo vya habari, katika awamu ya nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliahidi kuzitengeneza barabara kuu za Mji Mkongwe.

(a) Je, ahadi ile ipo mpaka leo.
(b) Serikali imechukua hatua gani kuona kuwa ahadi ile inatekelezwa.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ningependa tu tukumbushane kwamba awamu ya nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoa ahadi nyingi sana, naona ahadi nyingi hazikutekelezwa. Kwa hivyo kwenye hilo naweza nikasema kwamba wajibu wangu ni kwenda kufuatilia. Kwanza nione hiyo ahadi kwa maandishi, halafu niwaite na wale wahusika, niwaulize kwamba wanifahamishe, nifahamu kwa nini hiyo kazi haikufanyika na ikiwa kweli nimehakikisha kwamba hiyo ahadi imetolewa. Mimi na Profesa Mbarawa tunafanya kazi kwa ukaribu sana, nitalichukua suala hili nitazungumza naye halafu na yeye pia ende akachunguze kunako rekodi zake atizame hiyo ahadi kama ilikuwepo kweli.

Na kama ilikuwepo nakuhakikishia kwamba nitafuatilia na nitakuja kukujibu kuhusu hatua ambazo tumechukua.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona kwa kunipa nafasi hii kuweza kumuuliza Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, Waziri wangu jembe pale kaka yangu ambayo anatupatia.

Mhe. Spika, kuna uvumi na maneno ambayo yanazungumzwa kuhusiana na jengo Beit-el-Ajaib, hata kwenye mitandao yanarushwa kwamba jengo lile lina matatizo ni bovu na linaweza kuhatarisha maisha ya wananchi ambao wanakuja pale na wageni wetu ambao wanakwenda kuangalia eneo lile.

Je, Wizara yake inalijua hili na kama inalijua, mikakati gani ambayo wameiweka kwenye kuhakikisha kwamba kabla hakujatokezea maafaa wanakabiliana nalo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ningependa kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ikiwa anazungumzia

hili jengo la Beit-el- Ajaib, basi ni kweli kwamba Wizara tunajua kwamba kuna matatizo kwenye jengo lile.

Tumeshazungumza na Mamlaka na Mamlaka wametuambiwa kwamba wamekwisha kuwasiliana na *UNESCO-Paris*, ili wakubali ile michoro ambayo tumeitengeneza katika kulitengeneza lile jengo sio kulijenga upya tuhakikishe kwamba halianguki.

Mhe. Spika, hiyo ni kweli Mhe. Mwakilishi hatari ya jengo lile kuanguka ipo. Mfano umewahi kutokezea kwamba kuna eneo fulani kulivunjika. Sasa katika harakati za kujaribu kulihifadhi jengo lile serikali iliwasiliana na Serikali ya Oman, kule Mfalme wa Oman alitupa ahadi kwamba Serikali yake itasaidia kugharimia matengenezo ya lile jengo.

Mpaka sasa hivi tumo katika mazunguzo nao na kinachokwamisha ni kwamba hatuwezi kwenda pale kulitengeneza lile jengo tunavyotaka sisi wenyewe. Ni lazima litengenezwe kufuata yale maagizo ya *UNESCO*. Kwa hivyo sasa hivi michoro ya jengo imeshapelekwa huko, tunasubiri watupe kibali ili twende tukaziombe hizo pesa kutoka kwa hao Waheshimiwa wa Oman halafu tuanza kazi.

Mhe. Spika, pia nilitaka ujue Mhe. Mwakilishi kwamba katika suala hili, tuliwahili kulizungumza kwenye Baraza la Mapinduzi na tulikubaliana kwamba iwapo itatokezea tatizo ya kupata msaada wa nje kulitengeneza lile jengo basi tutafanya mpango tutenge fedha zetu wenyewe ili tulitengeneze. Kwa hivyo nataka nikuhakikishie tu kwamba hilo tunajua na si uvumi ni ukweli na Serikali hii ya Dkt. Ali Mohamed Shein iko mbele kabisa kuhakikisha kwamba jengo lile halitoanguka na jengo lile tutalitengeneza na kuliimarisha ipasavyo.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Habari una maelezo ya ziada naona. Karibu Mheshimiwa unaweza ukarudi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Balozi Ali Karume kwa majibu yake mazuri na fasaha aliyoyatoa juu ya jengo lile la mambo ya kale.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Waziri wa Ujenzi, nataka nilithibitishie Baraza lako kwamba jana nimemuandikia barua Mhe. Waziri atupe ruhusa kuvihamisha vitu vilivyokuwemo katika jengo la Beit-el-

Ajaib. Tunahamisha kwa sababu *process* zote alizozieleza, wafadhili wa Oman wapo tayari na wameshathibitisha kulirejesha katika hadhi yake ya asili ili jengo lile liwepo vizuri.(*Makofi*).

Lakini vile vile *UNESCO* ambao wenyewe wanatupa yale masharti kupitia Mji Mkongwe wametupa barua ya kukubali kuendelea kulitengeneza jengo lile. Barua hizo zimepokewa ndani ya Wizara yake na zimepokewa ndani ya Wizara yetu na wakati wowote tutakapokamilisha kuhamisha vitu vile, basi jengo litarudia katika hali yake na watalii wetu wanaweza kuendelea kwenda kujionea mambo ya ajabu yaliyokuwepo pale.

Ahsatena sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa. Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Mswaada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya Mwaka 2015

(Kusomwa Kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Utangulizi:

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nimchukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi ya leo kutujaalia kuamka salama na kufanya shughuli zetu.

Pili niungane na wenzangu wote waliotangulia tokea tulipoanzia kikao hichi kuwapa pole wale wote waliopatwa na mtihani wa mafuriko ya mvua. Safari hii hata jimbo langu la Makunduchi limeathirika karibu nyumba 192. Kwa hivyo tukubali sote kwa pamoja tuwape pole na Inshallah Mwenyezi Mungu awape subra na Inshallah tutafanya jitihada ya kuhakikisha kwamba utaratibu unaandaliwa kuwapa kifutia machozi kwa upande wetu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, lakini la pili nitoe pole kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla kutokana na vifo vya wanafunzi wale ambao waliopata ajali ya basi

Arusha. Mheshimiwa naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehema mahali pema peponi, Amina.

Madhumuni ya Uwasilishaji

Mhe. Spika, madhumuni ya kuwasilisha Mswada huu ni kuwasilisha mapendekezo na marekebisho ya baadhi ya vifungu na kuongeza vifungu vipya katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar Nam. 4 ya Mwaka 2015, ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma yaani Tume ya Maadili.

Mhe. Spika, katika hatua ya awali ya utekelezaji wa sheria ya maadili ya viongozi wa umma imebainika kuwepo kwa ugumu wa utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Tume ya maadili kikamilifu. Hali ambayo imechangiwa na kukosekana kwa baadhi ya masharti muhimu katika sheria na kuwepo kwa baadhi ya vifungu visivyojitosheleza.

Sheria ya Maadili Ilivyoanza Kutumika:

Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitungwa mwaka 2015 na ilianza kutumika mwaka April, 2016 mara baada ya Waziri anayesimamia Maadili ya Viongozi wa Umma kuitangaza rasmi tarehemu ya kuanza kutumika. Hata hivyo katika Mkutano wa Tatu wa Baraza la Wawakilishi uliofanyika Septemba wa mwaka 2016 sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho katika jaduweli ya pili inaruhusu fomu ya tamko la mali ya madeni.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia mahitaji ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Maadili kuna haja ya sheria hiyo kufanyiwa marekebisho mengine muhimu kama ilivyoainishwa katika muhtasari huu.

Mhe. Spika, mependekezo haya yanatokana na mikutano baina ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi mbali mbali za seirikali wakati wa kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa maadili ya viongozi wa umma. Ufafanuzi wa vifungu vya sheria, maadili ya viongozi wa umma na utaratibu wa kujaza fomu yatamko la mali na madeni. Aidha mapendekezo haya yametokana na mambo yanayojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria kutokana na baadhi ya vifungu kutokuwa bayana au kutojitokeza.

Marekebisho Yanayopendekezwa:

Mhe. Spika, marekebisho yanayopendekeza yamehusisha maeneo yafuatayo katika sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma:

Sehemu ya Pili, Mapendekezo ya Marekebisho.

Kifungu cha 3:

Kwa kuondoa maneno yanayoleta utata kuhusu matumizi ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa viongozi wa Umma. Maneno haya ni viongozi wa kisiasa, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Viongozi wa Mahakama na Viongozi wengine. Yametumika kama sio sehemu ya kiongozi wa umma. Hali ya kuwa na wao wanaingia katika tafsiri ya maana ya kiongozi wa umma.

Kifungu cha 4:

Kuongeza maana ya maneno Taasisi ya Umma ambayo hayakuwa yamefanyiwa tafsiri katika Sheria. Pili kuweka tafsiri ya wazi ya maneno mgongano wa maslahi na mali na kuwa tafsiri hizo hazikutaja mambo muhimu kama mke, mume na watoto. Tatu kufuta tafsiri ya neno kiongozi kuwa Kiongozi wa Umma ya marekebisho haya. Kufuta naneno 'Kanuni za' yaliyomo ndani ya ufafanuzi ya neno Tume kwa sababu yanaleta mgongano wa kimaana na kuweka tafsiri inayojitokeza kwa maana ya maneno kiongozi wa umma kuwa maana iliyopo inaweka makundi matatu ya aina ya viongozi wa umma na hivyo kupelekea ugumu wa kuwatambua viongizi wengine ambao hawamo katika jaduweli la kwanza la sheria.

Kifungu cha 5:

Mhe. Spika, kifungu hiki kinabainisha majukumu ya Mwenyekiti, kuhusu usimamizi wa kazi ya Tume.

Kifungu cha 6:

Kufanya marekebisho nambari ya vifungu tofauti, kuweka masharti ya utaratibu ya upatikanaji wa Kaimu Mwenyekiti wa Tume.

Kifungu cha 9:
Kuweka muda wa utumishi wa Kamishna wa Tume kwa kuwa muda wa Kamishna haukuwekwa ndani ya sheria. Kuongeza kifungu kipya cha 9(a), 9(b)

na 9(c) kuhusu kujiuzulu au kuondolewa au kuwa wazi kwa nafasi ya Mjumbe wa Tume.

Kifungu cha 10:

Kuongeza kifungu kipya cha (10)(a) na (10)(b) kinachoweka majukumu na masharti ya kupatikana kwa Katibu wa Tume.

Kifungu cha 12:

Kwa kuongeza kazi ifuatayo katika kazi ya Tume ya Maadili. Kufanya uhakiki wa moja kwa moja wa taarifa za mali na madini za viongozi wa umma zilizowasilishwa kwa mujibu wa sheria ya maadili ya viongozi wa umma. Hii ni kazi muhimu ambayo inapaswa kuainishwa moja kwa moja ndani ya sheria.

Kifungu cha 13:

Kuongeza kifungu cha 13(2) kinachotoa uwezo kwa Tume ya Maadili kumtaka kiongozi wa umma au mtu yeyote kufika mbele ya Tume kwa ajili ya mahojiano.

Kifungu cha 16:

Kuongeza kifungu kipya cha 16(a) kinachomtaka kiongozi wa umma kutoa taarifa za ziada kuhuso tamko la mali na madeni aliyowasilisha Tume ya Maadili. Lengo ni kuipa Tume uwezo wa kutaka kupata taarifa za ziada kuhusiana na taarifa za kiongozi wa umma pale inapohitajika.

Kifungu cha 26 na 27:

Marekebisho ya baadhi ya maeneo yaliyokuwemo katika vifungu hivyo ni kama ifuatavyo:

Kifungu cha 31:

Marekebisho ya Kiuwandishi, kinarekebishwa. Kifungu cha 36,37:Marekebisho ya maneno pembeni (*marginal note*) katika kifungu cha 36 na yasomeke "taarifa ya fedha za mwaka" maneo hayo yanajirejea kama ilivyo katika maneno pembeni ya kifungu cha 36 na kifungu cha 29, lengo ni kutofautisha kati ya taarifa za fedha na taarifa ya utendaji wa tume.

Mhe. Spika, kuongeza kifungu kidogo cha (3) kinachoweka masharti ya kupatikana kibali cha Mahakama wakati wa uchunguzi wa *account* za *Bank*.

Kifungu cha 41:

Kufuta maneno baada ya idhini ya Baraza la Wawakilishi yaliyopo mwishoni mwa kifungu ili kumpa Waziri muhusika uwezo wa kuongeza au kupunguza orodha ya viongozi wa umma wanaowajibika kujaza fomu la tamko la mali na madeni na kufanya marekebisho yanayohitajika katika fomu ya tamko za mali na madeni.

Hitimisho

Mhe. Spika, Mswada huu unawasilisha mapendekezo, marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongo wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015 ili kukidhi mahitaji yaliyoainishwa na kuondosha upungufu uliokuwepo kwa kiasi fulani unaweza kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Maadili yaliyofanywa.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Spika, asante sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji. Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ameshawasilisha sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati inayoshughulika masuala ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Namuona Mhe. Mwantatu kwa niaba ya Mwenyekiti.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Ahsante sana Mhe. Spika, Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015.(*Makofi*).

Ahsante Mhe. Spika, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutujaalia afya njema, hekma na busara na kutuwezesha kukutana tena leo hii tukiwa katika hali ya salama na amani, kujadili Mswada huu muhimu katika nchi yetu, yenye ukomavu mkubwa wa kidemokrasia.

Mhe. Spika, aidha kwa niaba ya Kamati yangu naomba kutoa pole kwa wananchi wote walioathirika na mvua za masika ambazo zinaendelea kunyesha katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Tunaomba wananchi waendelee

kuchukua tahadhari na maradhi ya mripuko kwa kuimarisha mazingira yetu, kwa kuweka safi ili yawe salama kwa mda wote ambao mvua zinaendelea kunyesha.

Mhe. Spika, vile vile nadhani sitokuwa mwingi wa fadhila bila ya kushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu, kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya Mwaka 2015.

Mhe. Spika, baada ya kutanguliza shukrani hizo, sasa nitangulie kwa kusema kuwa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi inakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kuleta, "Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi Wa Umma Nam. 4 ya Mwaka 2015", mbele ya Baraza lako tukufu kwa lengo ya kufanya marekebisho ya baadhi ya vifungu ambavyo katika utekelezaji wa Sheria hiyo vimegundulika kuwa vinaleta utata.

Mhe. Spika, kimsingi kuna vifungu vya Mswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya Mwaka 2015 vimeundwa upya ili kuifanya Sheria Mama iweze kuleta urahisi katika utekelezaji wake na kutoa ufafanuzi zaidi wa vifungu vya awali.

Mhe. Spika, pia, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru wadau mbali mbali ambao Kamati yetu ilikutana nao kwa kuwashirikisha na kuweza kutoa maoni yao katika kuuboresha Mswada huu, ambao unakusudia kufanya marekebisho katika baadhi ya vifungu ambavyo katika utekelezaji wa Sheria hiyo vimegundulika kuwa na ukakasi. Hivyo, katika kwenda sambasamba na dhana nzima ya utawala bora ni dhahiri kwamba Sheria hii inahitajika ili kuweza kuijengea jamii kuwa na imani na viongozi wao.

Mhe. Spika, Kamati yetu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum iliupitia "Mswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya Mwaka 2015 ambapo marekebisho mbali mbali yalifanywa na kamati kwa umakini mkubwa na kuzingatia umuhimu wa Sheria hii yenye kujenga taswira pana ya utawala bora.

Mhe. Spika, vile vile napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa michango yao mikubwa waliyoitoa wakati wa kupitia Mswada huu, ambao

imeweza kuboresha marekebisho ya sheria hii, pia naomba uwatambue Wajumbe waliounda kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
5. Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf	Mjumbe
6. Mhe. Ali Khamis Bakar	Mjumbe
7. Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni	Katibu,
9. Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu

Mhe. Spika, aidha Kamati yetu kupitia Kanuni ya 106 (3) jadweli la kwanza katika Kanuni ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2016 imeweza kushughulikia vyema agizo la Kanuni hiyo na kuhakikisha kuwa, Mswaada huu umekuwa na ubora na wenye mazingatio yaliyo bora katika vipengele vyote ambavyo ni muhimu katika mustakbali wa uendeshaji wa Taasisi za kiserikali kwa kuzingatia mila na desturi ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huu, sasa kwa niaba ya Kamati yangu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi, naomba kutoa maoni yetu kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma namba 4 ya mwaka 2015 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kamati ilipokuwa inaupitia Mswada huu, ilitoa mapendekezo mbali mbali katika vifungu vilivyomo ndani ya Mswada huu. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni marekebisho katika tafsiri ya maneno ikiwemo maana ya neno “mali”.

Mhe. Spika, wakati tunajadili Mswada huu wa Sheria katika kifungu cha 4 cha Mswada huo katika tafsiri ya neno “mali”, Wajumbe wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum walikuwa na mawazo tofauti kuhusiana na tafsiri ya neno hilo. Wapo Wajumbe walioshauri maneno “mwenza wake au mtoto wake” yaliyojitokeza kwenye aya hiyo yaendelee kubaki na baadhi ya Wajumbe wamependekeza maneno hayo yafutwe.

Hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(8) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi naomba kuwasilisha pia maoni ya Wajumbe wa Kamati hii, walio wachache ambao hawakuunga mkono tafsiri ya neno **“**mali**”** ili Baraza lako Tukufu

liweze kuzijadili hoja mbili hizi kwa lengo la kupata tija iliyokusudiwa ya kuanzishwa kwa Sheria hii.

Mhe. Spika, Kamati pia imebaini kuna baadhi ya vifungu viko tofauti katika Mswada wa Kiswahili na ule wa Kiingereza, Miongoni mwa mapendekezo hayo ni katika ukurasa wa 5, Kifungu cha 11 kinachohusu **"**Kuongezwa kwa vifungu vipya vya 10 A na 10 B**".** Kamati inapendekeza kifanyiwe marekebisho katika kifungu cha 10A (2) (c) kwa kuongezwa maneno baada ya neno **"**uadilifu**",** liliopo mwisho wa aya hii ambayo yatakayosomeka, **"**katika utumishi wa umma". Lengo la marekebisho hayo ni kwenda sambamba na Mswada wa Kiingereza.

Mhe. Spika, vile vile, katika Sheria inayorekebishwa kupitia Ukurasa wa 6 Kifungu cha 13 kinachohusu **"**Marekebisho ya kifungu cha 13" Kamati inashauri kufanyiwa marekebisho katika aya yake ya (d) kwa kuongezwa maneno **"**kwa njia ya mdomo au maandishi**"** baada ya neno **"**kuhojiwa**"** liliopo baina ya neno "ya" na "kuhusiana", kutokana na kukosekana kwa maneno hayo ambayo yanaainisha ni njia gani itumike katika kufanya mahojiano kama yalivyotumika katika Mswada wa Kiingereza.

Mhe. Spika, **v**ile vile kamati yetu inaendelea kushauri kuwa katika Ukurasa wa 7 Kifungu cha 17 kinachohusu **"**Marekebisho ya kifungu cha 31**"** kinafanyiwa marekebisho katika maelezo yaliopo chini ya aya (d) kwa kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo:-

"ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua milioni moja na isiyozidi milioni tano au atatumikia adhabu ya kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili faini na kifungo."

Mhe. Spika, Kamati yetu inapendekeza kufanyiwa marekebisho aya hii ili kuweza kulingana kwa adhabu na kosa lililofanyika, kwani katika marekebisho yaliyopendekezwa, adhabu iliyowekwa ya kifungo isiyopungua mwaka mmoja na isiyozidi miaka miwili na faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja na isiyozidi Shilingi Milioni Mbili ni ndogo sana kulingana na ukubwa wa kosa lenyewe.

Mhe. Spika, katika Sheria inayorekebishwa katika ukurasa wa 7 Kifungu cha 20 kinachohusu marekebisho ya Kifungu cha 41 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "baada ya idhini ya Baraza la Wawakilishi" ambayo yamejitokeza mwishoni mwa kifungu hiki. Kamati yetu

inapendekeza kifungu hiki kibakie kama kilivyo katika Sheria mama ili kupata ridhaa ya Baraza la Wawakilishi katika kufanya marekebisho ya Sheria hii, kwani hiki ndio chombo cha kutunga Sheria chenye kuwakilisha maoni ya wananchi.

Mhe. Spika, baada ya kueleza haya machache nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa hekma na busara walizojaaliwa nazo waitumie fursa hii, ili waweze kutumia uwelewa wao kuuchangia na kuurekebisha Mswada huu kwa kutoa maoni yatakayosaidia kuuboresha na hatimaye kuupitisha na kupata ufanisi katika utekelezaji wake.

Mhe. Spika, Naomba kuwasilisha

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwantatu ambayo ni Makamo Mwenyekiti wa hiyo kamati.

Waheshimiwa Wajumbe nina wachangiaji wawili na mchangiaji wa mwanzo atakuwa Mhe. Rashid Makame Shamsi ambaye atafuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikiwa mchangiaji wa mwanzo kabisa wa Mswada huu wa Marekebisho wa Sheria ya Maadili, lakini vile vile nichukue fursa hii ya kumpongeza na kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Wizara hii ya Sheria, Katiba, Utawala Bora kwa uwasilishaji wake mzuri wa Mswada huu wa marekebisho pamoja na watendaji wake wa Wizara inayohusika.

Lakini vile vile nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati inayohusiana na Sheria na Utawala Bora, lakini hususan muwasilishaji kwa niaba yake Mwakilishi wa Viti Maalum Walemavu ndugu yangu Mwantatu, kwa ufasaha na uweledi wake katika maelezo yake.(*Makofi*).

Mhe. Spika, ukweli Mswada huu umekuja wakati mfupi tu baada ya sheria hii kutungwa na kutumika. Sheria hii tunaambiwa ilitungwa 2015 na mwaka jana mwishoni Mswada huu ukawekwa mezani na leo tunaujadili. Ukweli ni muda mfupi sana na suala la Sheria ni suala zito kwa sababu linagusa wananchi. Mswada iwapo kwamba au Sheria ambapo haikutumika muda mrefu baadae inaletwa katika chombo kama hiki cha Sheria, maana yake kuna matatizo ambayo yalishinda au yalileta tabu katika utekelezaji wake.

Mhe. Spika, lakini tukumbuke kwamba tunapotumia muda mfupi wa matumizi na hatimae kufanya marekebisho hizi ni gharama, hizi ni kodi za wananchi, tunalazimika sana tunapopitia au tunapotunga Sheria basi tuwe na mazingatio makubwa sana ndugu Wajumbe ili kuepuka kutumia fedha za wananchi katika kuleta marekebisho ambayo yanakuwa ya muda mfupi. Kwa kweli suala la Sheria linahitaji umakini sana.

Mhe. Spika, kwa hiyo niwaombe ndugu Wajumbe vile vile hivi sasa Mhe. Spika anasema kuna watu wawili, lakini niwaombe ndugu Wajumbe tuweze kutoa michango yetu ya kuweza kuona kwamba Sheria hii tena isije ikawa inakwenda kutumika mwaka wa pili, wa tatu inarudi tena. Niwaombe sana ndugu Wajumbe tuchangie sana ili sheria hii sasa ikitoka iweze kutumika kwa muda mrefu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi nianze na wasi wasi uliojitokeza katika Ripoti ya Kamati. nianze na tafsiri ya neno hili la mali.

Mhe. Spika, katika sheria mama ilitolewa tafsiri kwamba mali ni kitu chochote kinachomilikiwa na kiongozi wa umma ambacho kina thamani na kinaweza kuuzwa au kutumika kulipa deni. Nimetoa tafsiri kwa Kiswahili inawezekana kisiwe sahihi kwa sababu Sheria ile iko kwa Kiingereza.

Sasa Mhe. Spika, tukija katika tafsiri ambayo imetolewa katika marekebisho, wenzetu wamepatwa na wasi wasi kwa sababu katika tafsiri hiyo imetaja "mwenza wake", inasomeka, maana yake ni kitu chochote kinachomilikiwa na kiongozi wa umma, mwenza wake na mtoto wake ambacho kina thamani na kinaweza kuuzwa na kutumika kulipia deni.

Mhe. Spika, hapa Wajumbe wa Kamati walikuwa na wasi wasi na mimi vile vile nina wasi wasi. Ninapenda niweke wazi na ndugu Wajumbe wa Baraza hili waitazame vizuri tafsiri hii. Kwanza nipendekeze kwanza neno, "mwenza". Neno "mwenza" katika tafisiri ya Kiingereza ya Mswada kuna neno *spouse.* Sasa *spouse* linatafsiriwa kwamba ni mke au mume. Sasa mwenza unapoenda katika Kamusi ya Kiswahili, mwenza maana yake ni mtu yeyote ambaye mnamiliki kitu pamoja au mali pamoja. Sasa kwanza hapa hii neno mweza tukienda katika Kamusi lina utata. Ningependa kama tutakubaliana iwe mke/mume, hilo halitakuwa na utata kuliko neno mwenza, kwa tafsiri ya neno *spouse* ya Kiingereza.

Lakini Mhe. Spika, kwa tafsiri ya "Kiongozi wa Umma", halafu leo kwenye tafsiri ya neno "mali" unamuingiza mke au mume na mtoto. Hapa unakuja wasi

wasi kwa sababu mali hizi ziweze kuja kulipa deni, *in case* kwamba kiongozi huyu wa umma amekumbwa na matatizo ya ubadhirifu pengine au wizi na akatakiwa kulipa. Sasa yeye fedha zake au mali yake ni kidogo, kwa tafsiri hii maana yake inaweza kumuingiza mke au kumuingiza mume wake mtu au mtoto wake, yaani mali zake. Sasa hapa kuna wasi wasi. Ningependa sana na huu ni wasi wasi wa Wajumbe ningependa sana tuitazame ili isije ikawaletea madhara wale wake zetu au waume zao au watoto wao juu ya mali zao.

Mhe. Spika, nikitoka hapo katika wasi wasi ambao wameuonesha vile vile Kamati, nije sasa katika ukurusa wa 4 kipengele hicho cha juu kabisa nambari 6 ambacho kinasomeka, "Endapo itatokea Mwenyekiti hatokuwepo Ofisini au atashindwa kutekeleza majukumu yake Rais anaweza kumteuwa kwa kipindi maalum mtu yeyote kuwa Kaimu Mwenyekiti ambaye atatekeleza majukumu ya Mwenyekiti'.

Mhe. Spika, katika tafsiri ya Kiingereza inasema, "*In the absence of the chairman or inability of the chairman",* mimi niko hapa kwenye "*In the absence of the chairman",* na hii tafsiri ya Kiswahili ambayo imetolewa. Nafikiri mantiki yake kidogo haijakaa sawa. "Endapo itatokea Mwenyekiti hatokuwepo", mimi ningependa isomeke kwamba,

"Endapo Mwenyekiti atashindwa kwenda kazini", hiyo nafikiri itakuwa inaleta mantiki. "Endapo Mwenyekiti atashindwa kwenda kazini au kushindwa kutekeleza majukumu yake", iendelee hivyo. Hapo naona itakuwa na mantiki nzuri kuliko tafsiri ya neno kwa neno ambayo imetumika.

Mhe. Spika, nije sasa katika ukurasa huo huo katika kipengele kinachohusiana na kufuta uteuzi wa Kamishna kwenye kipengele cha (b). Katika tafsiri ya Kiingereza, neno hilo ilikuwa ni, "*misbehavior".* Sasa *misbehavior* kwa tafsiri halafu kuna na *misbehavior* maana yake ni utovu wa nidhamu au utovu wa adabu, ndio ambao limetumika hapa. Lakini neno liliopo katika Kiingereza ni *misbehavior.* Ningependa sana neno hilo lisomeke sasa tabia mbaya au mwenendo mbaya, kuliko lilivyo hapo.

Lakini Mhe. Spika, nikija kipengele cha chini cha 9(b) linalohusiana suala la kujiuzulu kwa Kamishna. Mhe. Spika, katika *version* ya Kiingereza ya Mswada huu inaonekana *paragraph* moja tu ambayo ndiyo imeeleza, lakini hapa kuna *statement* mbili ambazo pengine inawezekana zinachukua muhtadha wa kutafsiri ili *paragraph* moja. Sasa mimi nahisi kwamba hivi vitu viwe vinaendana sambamba. Kama kule kuna *paragraph* moja basi na maelezo haya, *statement* mbili hizi ziwekwe na zinawezekana kuwa katika *paragraph* moja.

Mhe. Spika, nije sasa katika ukurasa wa 5. Katika ukurasa wa 5 kifungu kinachorekebishwa cha 10 (a), kifungu cha (b) ambacho kinasomeka "na uzoefu usiopungua miaka saba katika fani hiyo".

Mhe. Spika, katika *version* ya Kiingereza inasema, "*has high level of integrity in the public service"*. Samahani Mhe. Spika, katika *version* ya Kiingereza kuna neno la mwisho linalosomeka, "*in the related field"*. Sasa ningependa hapa isomeke sio katika fani hiyo lakini isomeke fani yenye uhusiano nayo au fani yenye kufanana nayo. Hilo ni muhimu sana.

Lakini katika kifungu (c) inasema mwenye kiwango kikubwa cha uadilifu. Sasa katika *version* ya Kiingereza inasema, "*has high level of integrity in the public service"*. Sasa neno, "*in the public service"*, katika tafsiri ya Kiswahili hiyo haipo. Ningependa hicho kifungu sasa kisomeke, "Mwenye kiwango kikubwa cha uadilifu katika utumishi wa umma", isomeke hivyo. Hapo itakaa vizuri zaidi.

Mhe. Spika, sasa nije katika ukurasa wa 6 kwenye masuala yanayohusiana na mambo ya taarifa za ziada, kwenye kifungu 16A kifungu 2 (b), kuna *statement* ambayo inasema, "Kiongozi wa Umma kufika mbele ya Tume kwa ajili ya kuthibitisha tamko la mali na madeni".

Mhe. Spika, katika *version* ya Kiingereza imesema in *order to verify his declaration on the asset*, hakuna neno "*asset"* and *debt"*, hakuna neno madeni. Sasa hapa kuna neno madeni limeingia.Tungependa kuona usahihi uko vipi. Kama madeni yanaingia basi na ile *version* ya Kiingereza ambayo ndiyo tunaifuata basi nako liingizwe na kama sivyo basi madeni hapa yafutwe ibaki mali.

Mhe. Spika, niendelee sasa katika ukurasa wa 7 kifungu ambacho kipo juu cha 31 (a), kuna maneno yanayosema, "anaye mzuiwa mtu anayetekeleza majukumu yake". Lakini katika *version* ya Kiingereza kuna maneno mawili yametumika "*obstruct or hinders"* ambapo tafsiri zake zinafanana kuweza kuweka pingamizi au kuzuwia. Ningependa maneno yote haya mawili yatumike katika kipengele hichi na yasomeke kwamba, "anayemuekea pingamizi au kumzuwia", kwa tafsiri ya ile ya Kiingereza.

Lakini tukija katika kipengele cha (d) ambacho kinasomeka anayetoa taarifa yoyote aliyoipata katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Kipengele hiki Mhe. Spika, hakimo kabisa katika *version* ya Kiingereza, kama hakimo na tume-*refer* kule. Sasa sijui inakuwaje. Ningependa sana kipengele

hicho kama hapa kimeongezwa basi itazamwe na *version* ya Kiingereza tuone kwamba hicho kifungu kinaingia.

Mhe. Spika, nije sasa katika kifungu cha chini hapo ambacho *statement* yake ya mwisho inasema kwamba faini isiyopungua shililingi milioni moja (1,000,000/=) na isiyozidi shilingi milioni mbili (2,000,000/=) au adhabu zote mbili, yaani kifungo na faini. Ningependa sana Mhe. Spika, hapo baada ya kifungo na faini ianze faini na kifungo kwa mujibu vile vile wa tafsiri ya Kiingereza.

Mhe. Spika, nije sasa katika kifungu cha 19 (b) kuna neno katika mstari wa pili kutoka chini, akaunti ya fedha. Lakini katika kifungu cha (a) kilizungumzia akaunti ya benki. Sasa ni vyema haya maneno mawili yawe na uwiano mzuri, kama tunatumia akaunti ya benki iwe ya benki na kama tunatumia akaunti ya fedha iwe akaunti ya fedha.

Mhe. Spika, baada ya michango hiyo mimi nikushukuru kwa nafasi hii ulionipa na niwaombe sana ndugu Wajumbe wauchangie Mswada huu na hatimae tuweze kuupitisha. Na mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia juu ya marekebisho ya Mswada huu.

Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi. Waheshimiwa sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said atafuatiwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed na Ali Suleiman Ali ajiandae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, nianze kukushukuru wewe kwa nafasi hii ulionipa lakini pia kwa niaba ya wananchi wangu ambao mimi ndio ninayewawakilisha katika Baraza hili, niweze kutoa mawazo yangu, fikra zangu juu ya marekebisho ya Mswada huu leo ambao mapendekezo yao pia yameletwa na Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Mswada huu. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa jinsi alivyowasilisha Mswada huu na mapendekezo yote.

Mhe. Spika, mchangiaji wa mwanzo alipochangia kwa kweli lazima nikiri amenifilisi au inawezekana atakuwa ametufilisi sote tutakaofuata hapa kutokana na utaalamu wake akionesha umahiri wake, akiwa kama *backbencher*, lakini pia kama ana Kamati mfukoni mwake, maana yake sio mchezo kuweza kuuchambua Mswada huu na marekebisho yake kwa jinsi alivyofanya yeye. Mimi nitasema kwa muda mfupi katika mambo ambayo na

utaratibu mzima ambao pia Mswada huu niulichangia mwaka jana na mapungufu.

Mhe. Spika, katika utaratibu wa jinsi ambao watumishi wa umma pamoja na viongozi wakuu ndani ya serikali wanahitajika kujaza zile fomu mwisho wa mwaka na kuziwasilisha kwa taasisi husika. Moja ambalo lilijitokeza kwa watumishi wa umma ni jinsi ya mume au mke ambaye ni mtumishi kwenda kudai *bank statement* ya mwenza wake. Lakini pia inawezekana kwa mume kuweza kujaza fomu hii na kudai *bank statement* kwa wake zake. Sasa hapa nataka niseme vitu viwili.

La kwanza kuna viongozi ndani ya utumishi wa umma lakini pia Wajumbe wa Baraza hili hili, hasa akinamama ambao wapo ndani ya utumishi wa umma na pengine pia Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi, walikataliwa kupewa *bank statement* na waume zao, kwa sababu *bank statement* unapoichukua kumkabidhi mtu pia inaanika undani wako, uwezo wako na ile akiba yako yote uliyokuwa nayo benki.

Lakini pia niseme utaratibu mzima wa kukabidhi hizi fomu katika utumishi wa umma. Sasa nina mapendekezo yangu mawili. La kwanza naomba sana kwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na Waheshimiwa wote wanapokabidhi fomu zao, wakabidhi kwa kiongozi mmoja muhusika mkuu ndani ya taasisi hii, ili kuhakikisha hizi taarifa hazivuji nje. Kwa nini nasema hivyo. Tumeona maeneo mengi unapokabidhi hizi fomu ndani ya Utumishi wa Umma inatoka katika eneo moja inakwenda eneo la pili, hatma yake unakuta fomu inapigwa picha halafu inarushwa kwenye mitandao ya kijamii. Ni aibu sana kwa serikali yetu kuona *bank statement* ya Waziri wetu inaanikwa nje hadharani kutokana na kwamba utashindwa kujua ni nani aliyemkabidhi hasa katika hizo fomu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, na hili hatusemi kama pale penye makosa, tunazungumza katika aibu nzima kuonesha kwamba Waziri wetu fulani, mali zake ni hizi, Katibu Mkuu wetu fulani mali zake ni hizi, mheshimiwa fulani mali zake ni hizi. Kwa hivyo naomba sana kwa heshima ya viongozi ambao wamo ndani ya Utumishi wetu wa Umma pamoja na Waheshimiwa wote wengine, basi utaratibu uwe kukabidhi kwa mtu mmoja tu ndani ya serikali ili tujue pale panapovuja kitu wa kumkamata au muhusika atakuwa ni nani, na ikiwezekana awe huyo huyo Katibu Mtendaji wa hiyo taasisi husika.

Mhe. Spika, pia nizungumze hili suala la *bank statement*. Mhe. Spika, wenzetu Bara walijaza hizi fomu na walipojaza hizi fomu hawakutakiwa kupeleka *bank*

statement ya muda wa miezi mitatu. Kwanza kupata zile *bank statement* zote ambazo yule mtu anahusika, lakini kenda kuzikabidhi kwa mtendaji ambaye hatumjui wadhifa wake ndani ya ile taasisi husika, anaweza kuwa ni karani wa kawaida kutokana na wingi wa kukusanya zile fomu. Maana yake sio mchezo kukusanya zile fomu zote katika kipindi cha miezi miwili mpaka mitatu, uchukue Utumishi wote wa Umma na viongozi wote pamoja na Waheshimiwa kwenda kuzikabidhi.

Mhe. Spika, sasa hizi *bank statement* mimi nataka nielewe unapojaza akaunti ya benki, ikiwa ni *NMB*, ikiwa ni *PBZ* tayari serikali hii ina uwezo wa kuzipitia kwa utaratibu wa kisheria kutambua pale penye makosa au wanataka kumchunguza mtu wataweza kujua tu, kwa sababu kuliko kwenda kupeleka *statement* za watu na kuanza kuangalia ya kila mtu. Kama wanahisi kuna watu muhimu wapeleke basi wapeleke. Hata mimi sina tatizo lakini tatizo ninaona tabu viongozi wetu ndani ya serikali Mawaziri na wengine kumkabidhi *bank statement* kwa mtendaji ndani ya serikali, halafu zinapita zaidi ya mikono mitano, pale ambapo panapotokezea *leakage* huwezi kujua ni nani aliyefanya lile kosa. Na huwezi ukafanya kazi au ukafanya uchunguzi wa kudadisi kwamba tuna wasi wasi ni huyu, lazima tuwe tuna uhakika ni nani anayehusika. Kwa hivyo mimi naomba sana kama wanaweza waangalie utaratibu wa kutambua zile benki zote zilizokuwepo ni ngapi, yule mtu ajaze akaunti ambazo anaziona *personal* pamoja na hisa alizokuwa nazo, pamoja na makampuni ambayo yote yanayohitajika kujaza aweze kuweka katika zile fomu.

Mhe. Spika, nataka nizungumze pia katika suala hilo hilo juu ya watumishi wetu wa umma. Mhe. Spika, kwa utaratibu uliokuwa unatumika mwaka huu kwa kweli nilipata unyonge sana kuonea watumishi wa umma hasa wanaotoka vijijini na maeneo tofauti nje ya Mikoa yetu. Mhe. Spika, waondoke shamba na maeneo tofauti kuja Mjini kupanga foleni kwenda kudai *bank statement* siku ya Ijumaa, inamalizika pale unaambiwa pengine mtandao uko chini au umeharibika, urudi tena wiki ijayo, unakuja tena unahangaika kutupa nauli yako na muda hutoweza kulikamilisha hilo.

Mhe. Spika, sasa mimi natoa rai hapa. Katika kujaza hizi fomu zote watafute utaratibu wa kujaza *quartely*, ikiwa kuanzia Januari mpaka Machi watapokea za wizara ambazo zina wafanyakazi wengi kama ni Afya na Elimu, kuanzia April, Mei na Juni watakuwa ni hawa, kuanzia Julai, Agosti na Septemba itakuwa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Mawaziri wote na pengine na viongozi wakuu halafu wengine wanamalizika.

Mhe. Spika, unapoweka *time table* utapunguza ule urasimu na wingi wa watu kuja kwa wakati mmoja kuvamia mabenki yetu, kujaza mafoleni na kuleta makaratasi kwa ujumla hatma yake pia wakati mwengine hata katika kuangalia kama vile zilivyojazwa kazi yao kama ipo sahihi na wapi penye mapungufu wataweza kuyaona na kutoa ushauri na utekelezaji wote. Mhe. Spika, hili litawasaidia wenzetu watumishi wa umma ambao wao makaazi yao wako nje ya Mikoa ya Mjini na kupata hizi huduma ambazo zinazostahiki.

Mhe. Spika, mimi baada ya hayo namalizia la mwisho kwamba ninapata wasi wasi juu ya uhakiki wa mali kwa ujumla, kwa sababu bado wananchi wetu uelewa wanapofanya manunuzi kama mfano ya magari au nyumba na mengineyo kutobadilisha jina la mmiliki aliyepita na kuhalalisha mmiliki aliyekuwepo. Viko vyombo vya moto ambayo inawezekana sana watumishi wa umma bado wanatumia lakini umiliki wake tayari umeshakuwa *transferred.* Sasa pale panapotokea utata lazima Sheria hii iweze kuwalinda, inawezekana sana mtumishi wa umma alikuwa na gari akaiuza ile gari yake lakini mmiliki mwengine hakufanya *transfer* ya kubadilisha jina. Kwa hivyo ni vizuri ili hii Sheria imlinde mtumishi wa umma ili kwamba ile mali sasa ameshaletewa mkononi aweze kujilinda yeye pamoja na mali nyengine zote anazotoa ambapo utaratibu wa kisheria yule aliyenunua hakubadilisha jina, basi Sheria hii na marekebisho iweze kumuangalia na kutambua au kutokana na maelezo atakayotoa.

Mhe. Spika, baada ya hapo nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na niseme pia naunga mkono yote marekebisho juu ya hoja na mawazo yangu haya niliyotoa. Nitamshukuru sana Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutoa maelezo ya kina na jinsi gani na utaratibu mzima kama nilivyozungumza wa hizi fomu ziweze kwenda kufanya kazi kuweza kuwasaidia watumishi wetu pamoja na viongozi wetu wakuu pamoja na Waheshimiwa tuliokuwepo hapa.

Ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Simai Mohammed Said. Sasa naomba nimwite Mhe. Mohammed Said Mohammed na yeye atupe mchango wake.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kuniona lakini kabla ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu. Vile vile nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri lakini nimpongeze sana na Mwenyekiti wa Tume hii ya Maadili kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya.(*Makofi*).

Mhe. Spika, Sheria hii ni Sheria ya karibuni, na Sheria hii imeundwa mwaka 2015 lakini imeanza kutumika 2016. Sasa utaona ni muda mdogo au ni muda mchache sana tumeanza kubadilisha Sheria, lakini ndio sheria. Kwa sababu Sheria sio Msahafu, chochote kinaweza kubadilika kwa manufaa ya wananchi au kwa manufaa wanayoyatumia.

Mhe. Spika, lakini kabla hatukubadilisha hivi tuone kwanza ubadilishaji huo una gharama gani. Gharama ya kwanza ni kuwa tunatumia pesa ya wavuja jasho. Mhe. Spika, hatutakiwi kutumia pesa ya wavuja jasho kila wakati tuwe na umakini. Nimwambie sana rafiki yangu Mwanasheria Mkuu ajitahidi sana kuwa tusilete kila wakati, yeye ni mweledi sana wa sheria na mimi namuamini, ni kiongozi mkubwa sana katika nchi yetu, ajitahidi sana tusitumie fedha za wananchi kwa mambo madogo kama hayo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi ninakwenda kwenye vifungu kama vinne kwa sababu wengi walishasema lakini hiki kimoja imebidi nikishereheshe kwa aina yake. Sehemu ya pili katika ukurasa wa 2 kwenye kifungu cha 4 kwenye sheria mama. Hapa inabadilishwa na kuandikwa “mali” na imetajwa maana yake ya mali. Sasa katika moja iliyotajwa maana yake ya mali ni mwenza au watoto.

Mhe. Spika, tabia ya wananchi wa Zanzibar, tabia ya Kiislamu pengine hatuambizani, tuna tabia ya kutokuambizana mali zetu. Ni vigumu mno sana mke akamwambia mume wake mali yangu hii lakini na waume kuwaambia wake zao mali yangu hii na hii. Sasa mimi nasema tu nipingane na kifungu hiki moja kwa moja, tusiwaweke wenza wetu si wanawake si wanaume. Lakini ikibidi kama tutaweza kuweka wenza tuweze kuweka *condition* au matamko ili ajaze yeye mwenyewe. Maana yake kuna siku inaweza ikatokea amekwambia uongo, aidha mwanamke au mwanamme amesema uongo na wewe umetia saini. Sasa lije jukumu lile liende kwake mwenyewe, lisiende kwako wewe. Hili ndio langu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, lakini moja tumeona hapa hata Kiongozi wetu Mkuu wa Serikali jana kasema kuhusu mambo ya *passport* wengine waliodai wasipewe hashughulikii, tumeona kweli wenza hawana maana yoyote. Kwa hivyo sioni haja hata moja ya kuweza kuweka hilo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, niende tena kwenye ukurasa wa 5, Nam.10(a) "kutakuwa na Katibu ambaye wa Tume atakayeteuliwa na Rais". Sasa zimetajwa sifa nyingi lakini moja ya sifa hii uzoefu wa miaka saba. Mimi naamini kwa sababu nilishiriki sana kwenye mjadala huo nikiwa kama mdau. Ninachoona na kinachonipa ukakasi, sijawahi kuona skuli yoyote ambayo inasomesha

experience sijawahi kuona. Sasa mtu kama hajafika miaka saba, uwezo anao kwa nini asiweze kuteuliwa. Mimi nadhani waone waangaliwe angalau basi nipendekeze kwa Mhe. Waziri, angalau yule mtu ambaye miaka mitano inatosha sana.

Mhe. Spika, jengine niende kwenye ukurasa wa 7 kwenye kifungu 31 pametajwa mambo mengi lakini moja imetajwa makosa. Kwenye kifungu Nam.17 na ukurasa wa 7 kilichoanzia ukurasa wa 6 yametajwa mambo yote lakini yametajwa makosa, faini. Mimi nadhani tuanze kwa sababu hili si la uhalifu, hatuwezi kuanza kifungo mwanzo, tuanze na faini kwanza, akishindwa basi ndio aende kwenye kifungu au vyote kwa pamoja. Lakini kwa sababu Sheria hizi tunazitunga tunatumia maneno makali. Leo Mhe. Abdalla Maulid Diwani anaambiwa Mwenyezi Mungu amuepushie mbali kifungo bila ya faini, na faini anao uwezo wa kulipa, anaweza akaanguka na akafa. Kwa hivyo tusitumie maneno makali sana. Mimi nasema tunaunda Sheria lakini tutangulize faini mwanzo na baadae tuweze kutanguliza kifungo.

Mhe. Spika, ukurasa huo huo katika kifungu cha 41, sheria mama inasema kwa idhini ya Baraza la Wawakilishi, lakini sheria hii utakuta leo imebadilishwa inampa Mhe. Waziri *loophole* ya kuweza kwenda. Mimi nasema tu ushauri wangu bado tunaweza tukakaa hapa hapa kwenye Baraza la Wawakilishi. Sababu wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nimeona wameanza kwenye Bunge kupeleka Sheria hii baada ya miaka mitano wamempa mamlaka Rais, baada ya miaka mitano wamempa waziri.

Mhe. Spika, sikatai na tunatunga Sheria. Leo tuna Waziri mzuri sana Mwalimu wangu Mhe. Haroun Ali Suleiman ni mcha Mungu, muadilifu na sifa zote nzuri anazo. Lakini kesho tunaweza tukampata Waziri jambazi, asiyejali maslahi ya wananchi, asiyejali watu, sio *fair*. Na hii mimi nataka niipinge hadharani, bado yabaki mamlaka ndani ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, twende kidogo kidogo, lazima tufunge *speed governor*, serikali isiende kwa kasi hapa. Mhe. Waziri tunakuomba sana punguza kasi yako, hapa twende kidogo kidogo na lazima tukufunge *speed governor* twende kwa *speed 20*, turudi tena kwenye Baraza la Wawakilishi ili basi tuweze kutoa idhini baada ya mambo yote yale.

Mhe. Spika, nikushukuru sana na mimi hayo ndio *concern* yangu kwenye Mswada huu mdogo ingawa wote wameanza kuusema na mimi siungi mkono hoja hii mpaka niweze kupewa majibu yangu haya. Lakini baada ya majibu yangu iridhike.

Mhe. Spika, nikushukuru sana.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa mchango wako. Naomba sasa nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu na kuchangia Mswada huu wa Maadili ya Viongozi kwa ufupi sana. Lakini nikushukuru tu kwa kuniona kwamba na mimi nipo na lazima niweke *hansard* vizuri juu ya hatma ya Mswada huu.

Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Rashid Makame Shamsi, kweli katufilisi na mara nyingi mimi Barazani nikisimama hutaka kuwa wa mwanzo ili mengi niyapate maana ukichelewa watu wameshayachukua. Lakini tunampongeza kwa dhati kabisa kwa sababu kazingatia kila kitu kinachofaa na kaeleza busara zake ili tufanikiwe katika harakati zetu juu ya Mswada huu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, bahati nzuri Mswada huu ulipitishwa mwaka 2015 Baraza lililopita, sisi wengi tulikuwa hatumo katika Baraza hili. Lakini nitoe indhari kwamba nakumbuka mwaka 1995 nilipoingia katika Baraza la Wawakilishi, mwaka 1996 tulitunga Mswada wa mambo ya Maliasili, ukichukua mchanga bila ya kibali gari lako linakamatwa, ukichukua mawe, ukichukua mambo yote ya asili kinyume na taratibu basi utakamatwa. Mhe. Spika, yalimkumba Mjumbe mwenzetu katika Baraza hili, gari lake liliwahi kukamatwa na alikataa kata kata kwamba Mswada huo haujui yeye. Lakini kwa bahati kwa kuwa mimi alikuwa rafiki yangu sitaki kumtaja watu watacheka, nikamwambia nenda kwa Mwanasheria Mkuu; alipokwenda alipoukuta alikamata kichwa akaona looh! kumbe kweli.

Mhe. Spika, sasa inapotungwa Miswada hii lazima tuangalie kwamba sisi ni watungaji wa sheria, lakini kuna jamii inatutegemea huko nyuma kwamba wao si watungaji sheria lakini itawaandama au itatuandama pamoja. Mhe. Spika, madhumuni ya kusema hayo Sheria kama hii ingelikuwa vizuri kwanza, wafanyakazi wote au viongozi wa taasisi mbali mbali wakapatiwa semina au wakapatiwa elimu, kwa sababu mtu anaweza kuingia pahala bila ya kujitambua.

Mhe. Spika, pia kupewa Mswada huu na yeye akaujua ilikuwa vizuri, viongozi wetu katika serikali yetu au taasisi za umma zote tulizokuwanazo wakapatiwa elimu kwamba kuna moja, mbili, tatu linakuja, na wao wakawa wadau wa mwanzo kutoa rai na maelezo yao. Kwa sababu tuliokuwemo humu sisi sote sio wanasheria au tutajua sheria, lakini tunao waliokuweko nje au katika taasisi

zetu wanajua kuliko sisi tuliokuwemo humu. Mimi ushauri wangu ulikuwa huo lakini kwa kuwa hili limepita, sasa tulitafutie busara liende kutusaidia huko mbele tunakokwenda.

Mhe. Spika, nikiri kwamba kila mtu ana mali yake, mwanamke ana mali yake, mwanamme ana mali yake. Nachukulia katika Wajumbe wa Baraza hili sote tuliopo hapa, wengine wanawake, wana waume zao na sisi wanaume tuna wake zetu. Lakini kupata somo au fedha ya mwenza, kama ilivyosemwa tutumie neno 'mwenza' ngumu. Kuna mwengine anakuamini Shihata mwengine hakuamini. Lakini na vile vile kuna mwengine mfano Mhe. Bahati Khamis Kombo anaaminiwa yeye, siku nyengine mume hamuamini mtu, yote yanatokea Mheshimiwa hayo.

Kwa hivyo, niseme tu kwamba tunapokwenda kutafuta *bank statement* huko benki, wafanyakazi wana kiapo chao. Sijui ufanye kitu gani hata upate ule ukweli kwa sababu akikwambia wewe una kiasi fulani huyo kasaliti kazi yake. Na hii ilikuwa patashika kubwa imetokea, kila mtu anapokwenda mimi nataka *statement* yangu napewa, nataka ya mke wangu, anakwambia mimi sitoi. Ndio nikasema kwanza ilikuwa elimu ndio jambo la msingi kabla ya hii Sheria haijapitishwa.

Mhe. Spika, na hii nasema sio utani kwa sababu naweza kuwa na mwanangu niliyemzaa, nikamwambia mtu ninayemjua katika benki bwana wee! nipe *bank statement* ya mtoto wangu, akanambia aah! kwa maadili yetu sisi haiwezekani. Kwa hivyo niseme hii Sheria nzuri lakini inataka kuangaliwa kwa tahadhari, lakini kwa kuwa imeshaletwa na inafanyiwa marekebisho, tuiweke vizuri ili kunusuru matatizo yasitokee kwa viongozi wetu wa umma katika nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine niseme tu kwamba uhakiki wa mali ni jambo moja na utumiaji ni sehemu ya pili. Mimi nina nyumba zangu tatu au mbili mfano, lakini nimekaa nimeona nyumba moja nauza, huku umeshaihakiki na kule inajulikana Shihata ana nyumba mbili. Je, leo nikija kutafutiwa ule ufumbuzi alitwambia ana nyumba mbili, mbona moja, kadanganya itakuwaje hapa. Maana huu ni uhakiki lakini nina shida mwenyewe nyumba yangu nimeuza, katudanganya huyu.(*Makofi*).

La pili, mimi nina nyumba tatu. Katika nyumba tatu hizi moja nilikuwa mimi na mwenza mfano. Hii sijui itakuwaje. Mimi bado nasema masharti ya Mswada huu bado magumu. Lakini kwa kuwa tumepitisha tunafanya marekebisho, tutafute ubora zaidi. Lakini mali ni kitu ambacho hakikai moja kwa moja.

Mhe. Spika, kwa mfano mimi nina shilingi zangu milioni tatu benki, nimekwama leo nikenda kutoa shilingi milioni mbili, imebakia shilingi milioni moja. Lakini uhakiki huyu katwambia ana shilingi milioni tatu, nyengine ziko wapi? Na hili lizingatiwe. Vyenginevyo kwa sababu pesa ni matumizi au mali ni matumizi vile vile, unaweza kuwa nayo sasa hivi, unaweza kuitoa na unaweza kuongeza. Mhe. Spika, alitwambia ana shilingi milioni tatu, kumbe ana shilingi milioni kumi kadanganya. Na hii si ya kila siku kama unakwenda kuripoti kwa taasisi hii kuwa leo nimeongeza katika orodha niliyoleta nilileta shilingi milioni zangu nane, lakini kumbe nina shilingi 15 watasema ulitudanganya. Sasa mambo haya Sheria ni msumeno na Sheria tukishaitunga ndio imetungwa. Mheshimiwa ulitudanganya ulitwambia una shilingi milioni nane kumbe shilingi 13 milioni. Na hilo tatizo liangaliwe. Lakini kwa kuwa Mwanasheria yupo na atakuja kutupa taarifa huko mbele atatusaidia kwa mambo mengineyo.

La mwisho Mhe. Spika, tatizo letu katika nchi yetu narudia tena wananchi wetu wengi bado hawaelewi mambo ya Sheria. Naomba mambo kama haya ambayo yanayogusa jamii yote, yaani watendaji wetu wote, yaani maadili ya viongozi yanaanza kwa viongozi wote, bado tukubali kwamba tukitoa Sheria hizi basi wale watendaji wetu wote wazipate, kuanzia ngazi ya Masheha, nani wote wawe nazo. Kwa sababu vyenginevyo Mheshimiwa hata tukifanya marekebisho ni vyema na wao wakapatiwa marekebisho yale, kwa ajili ya usalama au mtiririko wa masharti ya Sheria hii ili wasiende kujiyumbishs ua kuingia katika pahala pasipofaa.(Makofi).

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, niseme mimi moja kwa moja kwamba Mswada huu naukubali, lakini naomba taaluma itolewe kwa wenzetu, tukitoka hapa wajue kila kitu kwamba umetoka Mswada huu wa mwanzo lakini marekebisho yake yamekuja ya pili, wapatiwe viongozi wote wa umma ili wajue taratibu nzima zinavyokwenda kwa usalama wao.

Nashukuru Mhe. Spika, naukubali Mswada kwa asilimia mia moja. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Naomba nimwite Mhe. Mwanasheria Mkuu kabla sijamwita mtoa hoja.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa ili angalau kutoa ufafanuzi kwenye maeneo machache ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyazungumzia.

Kwanza na mimi naunga mkono hoja marekebisho ya Mswada huu kwa asilimia mia moja. lakini la pili nimshukuru Waziri kwa kuleta marekebisho haya. Haya ni ya pili kama ambavyo wamesema Waheshimiwa Wajumbe, lakini hiii inaonesha kwamba sheria hii nafanyiwa kazi, haya ndio matokeo yake. Kama sheria hii inafanyiwa kazi na pale inapofanyiwa kazi yale mapungufu yanapoonekana ndio inatubidi tuje tufanye marekebisho.

Mhe. Spika, sasa tunapokuja kufanya marekebisho Waheshimiwa Wajumbe msione kama hatuzingatii au hatutafakari kama anavyofanya mabadiliko nayo yanagharimu muda, yanagharimu fedha, maana pia tuna-*print*. Lakini inabidi na ndio uendeshaji wa Sheria ulivyo. Kama Sheria yoyote inapotungwa lazima ifanyiwe marekebisho na sheria unapoitunga unajua ubora wake au mapungufu yake pale unapoanza kuifanyia kazi.

Sasa Sheria hii imeanza kufanyiwa kazi mwaka 2016 na hayo ndio mapungufu ambayo tumeanza kuyaona. Sasa ili twende vizuri kutekeleza masharti yaliyomo ndani ya Sheria hii, inabidi kila inapohitajika haja tuje kufanya marekebisho. Sasa haya yataendelea sijui lini tutakuja tena lakini itakapobidi kufanya marekebisho basi tutakuja tena na Mhe. Spika.

Lakini la pili niwashukuu Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na mimi kwa nafasi yangu, naomba nikubaliane na yale yote ambayo Kamati imeyapendekeza. Nadhani wamefanya kazi nzuri sana na hili pia litajibu lile ambalo amelitaja Mhe. Mohamed Said Dimwa la kifungu cha 20 kama kibaki hivyo hivyo. Na mimi nakubaliana naye na wengi watakumbuka wakati tunapotunga Sheria hii mwaka 2016 hoja zilizokuwepo nyingi zilikuwa ni kama utekelezaji wa Sheria hii umo kwenye zile fomu ambazo zimo ndani ya Sheria hii, wala sio vile vifungu ambavyo vinatajwa. Kwa hivyo nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe kama utaratibu uliopendekezwa kwenye Sheria mama ubaki vile vile kama ulivyo.

La pili, ni hili ambalo Mhe. Rashid Makame Shamsi amezungumza na yeye nikubaliane naye sana, amefanya kazi nzuri na ameonesha umahiri wake na ameonesha kwamba anachukua muda wa kusoma na kupitia Miswada hii ambayo tunaileta kwa *version* zote mbili. Kwa hivyo namshukuru sana na mengi ambayo ameyasema nakubaliana nayo, isipokuwa lile la tafsiri ya mali. *Ofcourse* na hoja ambayo imewekwa ni kwamba sasa anaongezwa mwenza.

Kwanza nikubaliane naye kwamba ni vyema ili Sheria isomeke vizuri ni vyema itajwe mume au mke. Na mimi nakubaliana naye, ndio maana tunafanya tafsiri ya hizi Sheria ili kuondoa utata au ukakasi ambao unaweza kutokea wakati mtu

akisoma ile Sheria. Sasa ili isomeke vizuri basi na mimi nakubaliana naye ni vyema isomeke tu, mume au mke, au na watoto. Nadhani itakuwa imeondoa ule utata ambao umejitokeza. Lakini kwa nini tumeongeza mke au mume?

Mhe. Spika, kwa sababu ndani ya Sheria mama ilikuwa tayari kuna vifungu ambavyo vimetaja *spouse,* lakini kwenye tafsiri ilikuwa haikueleza neno *'spouse'*. Sasa ndio maana tukafanya marekebisho ya kwenye tafsiri ili na neno mke au mume lijitokeze kama ambavyo limejitokeza kwenye Sheria. Natambua sote hapa tungependa kama tusiorodheshe mali za wake zetu au mali za waume zao. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, sote tungependa iwe hivyo lakini tunatambua unapokuwa kiongozi wa umma, inakuja na gharama yake. Na moja ya gharama yake ni hiyo kwamba lazima uwe muwazi, lazima uoneshe, lazima watu wakupime kile ambacho unacho kinakwenda na kile ambacho unakipata. Lakini na sote tunatambua kwa nini hiki kimewekwa kwa sababu ilikuwa ni tabia na mtindo kwamba kiongozi wa umma anadhani ni yeye tu. Kwa hivyo wengine walikuwa wakipeleka kwa wake, kwa watoto. Sasa ili kuondoa hiyo dhana ambayo inaweza kujengeka, ndio maana Sheria sasa zimekuja kuweka wazi kwamba jamani hapana, unapokuwa kiongozi wa umma basi ujue kama kuna mambo mengine lazima yakutafautishe baina ya wewe kiongozi wa umma na yule ambaye yuko nje hakuingia kwenye uongozi. Moja ya gharama hizo Mhe. Spika, ni hizi lakini haikatazwi benki yako kuwa na kiasi chochote cha fedha, uwe nacho chochote ambacho utakuwanacho lakini utapoulizwa umekipataje ni taarifa zinazotakiwa zitoke.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe wasiogope kwamba labda akaunti ya Mhe. Waziri wa Afya itakuwa imenona au ya Mhe. Waziri wa Ujenzi itakuwa imenona au ya Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf itakuwa imenona, akaogopa kama kwa nini sasa nikipeleka *bank statement* yangu itaonekana akaunti yangu imenona. Tusiogope yanayotakiwa ni maelezo, utahojiwa umeipataje, kipato chako ni kipi, aah! mimi kipato changu ni hiki lakini mimi nafanya hivi, mimi nina kampuni, mimi nimerithi, nimefanyaje ndio maelezo tu yanayotakiwa. Lakini haikatazi kuwa na kiasi chochote cha mali Mhe. Spika. Kwa hivyo, niwatoe was iwasi Waheshimiwa Wajumbe.(*Makofi*).

Mhe. Spika, lakini na hii pia inatushajihisha tuwe wazi huko majumbani, *bank statement* hizi tu-*share* huko majumbani lazima wajue, unacho kiasi gani na wewe lazima ujue na yeye anacho kiasi gani. Ndio mambo yalivyo Mhe. Spika, lazima tu-*share*, lazima tuwe wawazi, ndio mambo yenyewe yalivyo. Sasa Sheria hii ndio inatuthibitishia tuwe hivyo kwamba tuache ile hofu, sasa una

hofu ya nini, yule mkeo na huyu mume, una hofu ya nini, tumia tu na yeye ajue kama mume wangu nikihitaji buibui jipya asiseme akaunti haina kitu ipo, akitaka gari ajue ipo ukamnunulie tu.

Mhe. Spika, lakini kiujumla ninavyotaka kusema ni kwamba niwatoe hofu Waheshimiwa Wajumbe kwamba haina dhamira ya kuingilia *privacy* ya mtu, lakini kinachotakiwa ni taarifa angalau ziwe wazi za kiongozi wa umma. Pia ukisoma Sheria yenyewe hata upatikanaji wa ile taarifa ni lazima mtu akaombe kwa sababu hiyo hiyo, kama Sheria imezuwia taarifa za viongozi kuwa wazi. Hata yale majina yanayotangazwa hayatangazwi na zile *attachment* ambazo wamepelekwa, ni majina tu ya nani ameshatangaza mali zake.

Sasa ukitaka kujua Mwanasheria Mkuu amepeleka nini, inabidi upeleke maombi kwa mwenyekiti na maombi atayazingatia na ama atakubali au atakataa kukuonesha Mwanasheria Mkuu kwenye *declaration form* yake amejaza ana nini, ameeleza nini. Sasa niwatoe hofu kwamba hata yale majina ambayo tunayatoa kwenye Gazeti Rasmi na tumeshaanza kuyatoa hayapelekwi na *declaration forms* ambazo Waheshimiwa Wajumbe au Waheshimiwa Viongozi wameyapeleka, yanayopelekwa ni majina tu peke yake lakini mtu anapotaka taarifa inabidi hizi taarifa aombe kwa Mwenyekiti.

Sasa kiujumla na mimi Mhe. Spika, nakubaliana na hoja hii iliyokuwepo mezani na nakubaliana na mapendekezo ambayo Kamati wameyatoa na mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyapendekeza.

Nakushukuru sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Sasa naomba nimwite mtoa hoja Mhe. Waziri wa Katiba, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Sheria tafadhali.

Mhe. Wazri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru tena Mwenyezi Mungu kutujaalia kufika hatua hii ya sasa hivi. Lakini pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa namna unavyokiendesha kikao chetu.

Mimi niwashukuru sana na niwataje wote waliochangia marekebisho ya Sheria yetu hii. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Bi. Mwantatu Mbarak ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii kwa niaba ya Mwenyekiti Mhe. Machano Othman Said. Lakini niwashukuru sana Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya wamechambua sana,

wamefanya kazi kubwa. Muda mwingi sana sijapata nafasi kukaa na Kamati kuuchambua Mswada wa Sheria kama kipindi hiki Mheshimiwa, nashukuru sana nawapongeza na waendelee kutusaidia. Wajumbe wote walifanya kazi nzuri.

Pia naomba nitambue mchango mzuri sana uliotolewa na Mhe. Rashid Makame Shamsi, nadhani ameonesha kama ni *model* ya namna gani Mswada unavyotaka uchambuliwe, kachambua hatua baada ya hatua, kipengele baada ya kipengele, sentensi baada ya sentensi, *comma* baada ya *comma* na *full stop* baada ya *full stop*. Nampongeza sana. Sioni ajabu ni mwalimu na kasomeshwa na walimu. Kwa hivyo kafanya uzuri hongera sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, aidha natambua mchango wa Mhe. Simai Mohammed Said na yeye kachangia kwa kiasi chake. Mhe. Mohamed Said Dimwa kachangia vizuri, Mhe. Ali Suleiman Ali kama kawaida kachangia vizuri sana na *AG* namshukuru sana kwa kweli kaifanya kazi yangu iwe nyepesi na ndogo. Mhe. Mwanasheria Mkuu namshukuru sana kwa kunirahisishia kazi na aendelee kunisaidia kazi ndio majukumu yetu sote.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie mawili matatu tu. Kwanza kuna jambo nataka nilizungumze hapa, unajua Mhe. Simai Mohammed aliposema Mhe. Spika, kwamba kwenye mitandao *bank statement* za baadhi ya viongozi zilienezwa. Mambo hayo ukiyazungumza uwe na ushahidi nayo ni jambo zito kidogo ambalo kalitamka hapa Barazani na jana tumehimizwa sana hapa kwamba tutoe kauli na matamko ambayo yatakuwa yanasaidia hayajengi.

Sasa hili jambo alilolitamka hapa ni zito. Mimi naomba Mhe. Simai tafadhali aje anione na anioneshe ushahidi huo na kama kuna Afisa yeyote katika Tume hizi amehusika tutachukua hatua za kinidhamu pamoja na kumuondosha kabisa katika eneo lile na kuchukua hatua nyengine kubwa zaidi. Hili ni jambo zito sana amesema kwanza siamini kama hilo linawezekana, kwa sababu ni watu makini Mhe. Rais kamchagua Mwenyekiti, kawachagua Wajumbe makini na Seketerieti iliyokuwepo pale ni makini sana. Sasa kama wameanza kufanya hayo kama nimekuelewa vizuri basi naomba sana tusaidiane ili kuliweka sawa hilo lakini siamini hayo.

Lakini la pili nataka niseme jambo hili kama alivyozungumza Mwanasheria Mkuu kinachotafutwa hapa ni uwazi. Sisi kama ni viongozi tunaingia kwenye dhamana hizi, tukiingia tujulikane tulivyo tukiondoka tutajulikana tulivyo vile vile. Sasa ukianza kumuogopa Polisi lazima kuna jambo huwezi kumuogopa Polisi kama huna jambo. Kwa hivyo ninachowaomba sana Waheshimiwa

tuelewane haya masuala hayana nia mbaya, yana nia ya kutengeneza kinachotafutwa ni uadilifu, ukweli na kuwa na viongozi safi sana ambao wataendesha nchi kwa manufaa ya kuleta maendeleo kwa wananchi wetu, tusiwe na hofu jambo hili ni zuri.

Lakini Mhe. Mohammed Said Mohammed kazungumza jambo moja, anasema tufanye marekebisho ya Sheria ile sehemu fulani kwamba mamlaka yale yarudi Baraza la Wawakilishi asipewe Waziri. Kwa sababu Waziri kwa mfano leo tunaye Waziri anasema, kamtaja Waziri aliyekuwepo sasa hivi lakini tunaweza kupata Waziri akawa jambazi.

Mhe. Spika, mimi nataka nikuhakikishie hakuna Rais yeyote atakayemteuwa Waziri aliyekuwa ni jambazi. Mawaziri wanaoteuliwa wote wanapitia kwenye mikondo mingi sana. Mimi sijui kwa sababu siteuwi Mawaziri. Lakini nina hakika inafanyika kazi nzito na Mhe. Rais huwa anafanya juhudi kubwa ya kutafuta Mawaziri ambao amewaamini.

Mimi nampongeza Mhe. Rais, Mawaziri aliyewateuwa wote ni makini na sidhani kama atakuja Rais atateuwa Waziri atakayekuwa na tabia hiyo mbaya, huyo keshajiondoa mwenyewe na fomu yetu ya maadili inaeleza usiwe mlevi yote yameelezwa. Sasa hizi tabia zitajulikana kabla hujaingia huku, huwezi kuteauliwa. Namuomba sana Mhe. Mohammed Said nataka nimukakikishe kwamba amuamini Waziri atakayeteuliwa na Mhe. Rais ni Waziri makini hatokuwa na matatizo tena.

Mhe. Spika, baada ya hayo niwashukuru Waheshimiwa wote waliochangia na ushauri wao wa Kamati na mambo mengine yote tunayachukua na kwenda kuyafanyia kazi.

Ahsante Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono. Katibu kwa hatua inayofuata. Naomba nichukuwa nafasi hii kwanza niwahoji.

Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, kabla sijaendelea na hatua nyengine naomba niwaombe radhi Waheshimiwa wawili ambao wameleta michango yao kwa maandishi. Naomba niwatambue na niwashukuru sana wa kwanza Mhe. Asha Abdalla Khamis na Mhe. Shamata Shaame Khamis vile vile kwa mchango wao wa maandishi tunathamini sana.

Mhe. Spika, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya kurekebisha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar Nam. 4 ya 2015

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1	Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2	Kusomwa
Kifungu 3	Marekebisho ya kifungu cha 2
Kifungu 4	Marekebisho ya kifungu cha 3 pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nililisema lile suala la mali ikiwemo na mwenza. Namshukuru sana Mwanasheria Mkuu lakini namshukuru na Mhe. Waziri wamelizungumza vizuri. Hofu yangu ilikuwa hawa wenza nimesema wanaweza kutupa taarifa zao lakini wanaweza wasitupe taarifa zao ama kiwekwe kipengele waondoshwe ama wawekewe kipengele ambapo wataweza kujaza wao wenyewe. Sasa nataka kidogo nipate ufafanuzi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohammed Said Mohammed akiisoma ile Sheria mama utakuta kuna zile fomu ambazo zinatakiwa zijazwe. Sasa maana yake kwa watoto itabidi sasa wajaze ama atajaza mama ama atajaza baba, inategemea nani ni kiongozi wa umma. Lakini kwa mke au mume inavyotakiwa ajaze yeye mweyewe taarifa zake kwa sababu inatakiwa ile fomu pia itiwe saini kwa sababu na yeye anatoa taarifa yeye atakuwa a*ccountable* kwa zile taarifa ambazo amezitoa. Kwa hivyo nadhani utaratibu upo vizuri wa kisheria Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. hofu yangu iko hapa jana wakati tulichangia hotuba ya Kiongozi Mkuu wa Serikali Barazani, kuna Mjumbe alionesha nia yake ya kuweza kuwapa *passport* hawa wenza ili kuwa nao karibu. Sasa kwenye Sheria hii tumeanza kutaja wenza lakini kwenye manufaa mengine wenza hawapo. Mimi ningeomba tuwaondoe wenza kwa sababu wenza hawana maana yoyote. (*Makofi*)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mheshimiwa yale ya jana nisingependa kuyarudia na tumeshamaliza. Lakini kwa haya ya leo nadhani ufafanuzi ni huo kama nilivyoutoa, na nimuombe Mhe. Mohamed Said Mohamed kama akubaliane na mapendekezo ambayo yapo kwa sababu hayana dhamira mbaya yana dhamira ya kujenga na kuweka uwazi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, naomba twende katika kura kwa sababu sikubaliani naye, msimamo wangu ni ule ule.

Mhe. Spika: Sasa naomba kuwahoji wale wote wanaounga mkono kifungu hiki kipite pamoja na marekebisho yake kama yalivyoletwa na Serikali wanyanyue mikono yao, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuwa na kuafikiwa)

Kifungu 4	Marekebisho ya kifungu cha 3 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 5	Marekebisho ya sehemu ya Pili pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 6	Marekebisho ya kifungu cha 4
Kifungu 7	Marekebisho ya kifungu cha 5
Kifungu 8	Marekebisho ya kifungu cha 6 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 9	Marekebisho ya kifungu cha 9
Kifungu 10	Kuongeza vifungu vipya vya 9A, 9B na 9C pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11	Kuongezwa kwa vifungu vya 10A na 10B pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana katika kifungu cha 10A chini kabisa limetajwa Katibu wa Tume na uzoefu wake. Lakini nilipokuwa nikichangia nimesema angalau basi Katibu huyu awe na miaka mitano baada ya miaka saba, kwa sababu kuna wengine wamefika

miaka mitano lakini wana uwezo mkubwa sana. Tukiendelea miaka saba sijaona chuo chochote duniani ambacho kinasomesha *experience*. Sasa kama hatukuweza kuwapa kazi siku zote tutawafyekuza vijana wetu ambao wanaotoka Vyuo Vikuu ili wasiweze kupata kazi hii. Tusijenge mazingira tata.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu uzoefu miaka mitano baada ya saba yeyote kati yenu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed *of course* ni nzuri na sote tungekubali yafanywe hayo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, uteuzi wa Rais na hasa kwa viongozi hawa ukiisoma ile Sheria ya Utumishi wa Umma inataka *Senior Public Service* awe na uzoefu usiopungua miaka 15, ukisoma ile Sheria ya Utumishi wa Umma ambaye atataka uteuzi wa Mhe. Rais.

Sasa kwenye hii haikundikwa kuwa huyu mtu awe ni S*enior Public service* lakini tukaona miaka 7 kwa nafasi kama hii ni *reasonable* kwa mtu ambaye atafanyakazi kwenye Tume hii. Sasa sisi dhamira yetu ni hiyo kwamba tusiende mbali zaidi ya ile Sheria ya Utumishi wa Umma ambayo ilivyo na tusiwe mbali zaidi na Sheria ya Utumishi ya Umma ambayo ilivyo.

Mimi nadhani miaka 7 si miaka mibaya, nadhani miaka 7 ni *reasonable* Mhe. Mwenyekiti. Hata Mwanasheria Mkuu anatakiwa awe na uzoefu wa miaka 7.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu hata mfano ambayo yeye mwenyewe amejitolea. Kazi ya Mwanasheria Mkuu ni kazi pevu na nilizungumza katika mchango wangu kuwa namuamini sana ni mweledi wa sheria.

Lakini hii hakuna katika Utumishi wa Umma, huyu mtu anayechanguliwa tukaweza kufika miaka 7. Mimi naona tunaweka *loophole* kubwa na hakuna maelezo ya kina ambayo yanaweza kusababisha huyu miaka 5 tusiweze kumpa kazi, tunajiwekea mazingira magumu vijana wetu wanafanyakazi Vyuo Vikuu leo wanakosa kazi.(*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohammed Said Mohammed nataka atuelewe vizuri.

Kwanza Mwanasheria Mkuu namshukuru kwa majibu yake ni sahihi wala hakuna haja ya kuyaongezea mengine. Isipokuwa hii miaka mitano, saba, kumi, kumi na tano tujue, hebu twende kwenye *professional* yetu ya walimu. Mwalimu anayesomesha miaka miwili, mitatu, minne, mitano, hawezi kamwe kuwa sana na mwalimu aliyesomesha miaka saba, nane, tisa na kuendelea. Uzoefu unasaidia. Jambo hili zito la kuangalia minendo au maadili ya viongozi wetu, kuchagua mtu *just* kwa sababu ana digrii ya kwanza ya pili ya tatu, hajafanya kazi, ndio kwanza miaka mitano, bado haja *mature*.

Kwa hivyo, naomba tukubali na sisi kwamba miaka saba ndio tunaanzia na *in fact* hiyo miaka saba ndio tunampa lakini tutizame huku mbele itakuwa hatma yake itakuwa nini. Kwa sababu si jambo rahisi jambo hili lina fitina kubwa na linataka uadilifu wa hali ya juu. Kwa hivyo namuomba Mhe. Mohammed Said Mohammed kama kawaida yake nikimuomba jambo hakatai na hili alikubali tuendelee na hatua nyengine leo Ijumaa tunafukuzia kusali.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, namuheshimu sana kupita kiasi mwalimu wangu Mwalimu Haruna na nimemfahamu vizuri. Lakini nataka nimpe mfano mmoja kabla sijalikubali hili jambo.

Mhe. Salim Ahmed Salim alipewa Ubalozi ana miaka 21. Sasa leo naona tunaweka hapa vipingamizi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hawa *graduants* wote wamejua nini nia yangu ninavyowatetea. Tuendelee kwa sababu namuheshimu mwalimu wangu.

Kifungu 12	Marekebisho ya kifungu cha 12
Kifungu 13	Marekebisho ya kifungu cha 13 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14	Kuongezwa kifungu kipya cha 16(A)
Kifungu 15	Marekebisho ya kifungu cha 26
Kifungu 16	Marekebisho ya kifungu cha 27
Kifungu 17	Marekebisho ya kifungu cha 31pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilisema tunaweza tukawa tunaweka maneno makali sana ya sheria. Lakini nikasema sikumsikia mwalimu wangu kujumuisha hili tuanze basi kwanza kuweza kuweka faini na baadae twende kwenye kifungo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, hili tulikubaliana hata kwenye Kamati kwamba tuweke kwana faini halafu baadae ndio kifungo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Naunga mkono hoja.

Kifungu 18	Marekebisho ya kifungu cha 36
Kifungu 19	Marekebisho ya kifungu cha 37 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 20	Marekebisho ya kifungu cha 41pamoja na marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa kwa sababu muda tuliokuwa nao tunahitaji kuongeza muda mchache sana ili kuweza kukamilisha hii kazi sasa hivi na kwa mamlaka niliyopewa naomba nizidishe kama dakika mbili tatu tu ili tulikamilishe hili halafu baadae tutakuja tena jioni saa 11:00 kamili kukamilisha hilo lilibaki kwenye *order paper*. Baada ya hapo Mhe. Waziri sasa nikwite.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, kwanza naomba kidogo niweke sawa jambo fulani ambalo limejitokeza hapa inawezekana kibinadamu wakati Mhe. Simai Mohammed Said anachangia alizungumza suala lile la Mawaziri na Makatibu Wakuu kwamba wawe na mahali maalum kupeleka fomu zao na inaweza ikaja kutokezea kaja kutokezea mtu akaja akatoa taarifa zile kwenye hadhara kwa watu au mitandao, alichokusudia yeye kwamba alikuwa anatoa tahadhari tu sio kwamba kasema kwamba kuna mtu. Kwa hivyo, naomba niliweke sawa kidogo hilo.

Baada ya hayo Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 2017

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 2017 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Muswada wa sheria ya serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Ahsanteni Waheshimiwa, nafikiri mpaka hapo tutakuwa tumekamilisha zile hatua zote za kuupitisha mswada.

Waheshimiwa Wajumbe naona bado tumo ndani ya wakati bado kama dakika moja. Naomba niitumie dakika moja hii kutoa matangazo. Kwanza kabisa Waheshimiwa naomba niwakumbushe kwamba kesho tarehe 13/05/2017 kutakuwa na ile dua ambayo tulikuwa tumeizungumza kwenye *briefing* na *caucus* ambayo itafanyika katika msikiti wa Malindi kuanzia saa 2:00 usiku.

Lakini pia siku ya Jumapili kuna semina ambayo inahusiana na masuala ya bajeti siku ya Jumapili. Kwa hivyo, nakukumbusheni kwamba hiyo semina bado ipo, kwa hiyo tutakuja kushiriki kama kawaida.

Baada ya matangazo hayo machache naomba sasa nisitishe shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka saa 11:00 jioni leo.

(Saa 6:00 mchana Kikao kiliakhirishwa mpaka saa 11: 00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

KAULI ZA SERIKALI

Hotuba ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2014/2015

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uzima na afya na kuweza kukutana jioni hii tena tokea tulipoagana pale mchana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kuzipokea na kuzifanyia kazi ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka 2013/2014.

Aidha, kutokana na jitihada zilizochukuliwa za kuimarisha Utawala Bora, pamoja na hatua mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zinazopelekea kuimarika kwa uwajibikaji na nidhamu katika matumizi ya fedha na rasilimali ya umma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima nachukua fursa hii kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali, ilitekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa kukagua mahesabu ya mwaka 2014/15 kwa wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na taasisi zake. Matumainio yangu ripoti hizi zitaonesha sura halisi na mwenendo mzima wa udhibiti wa masuala ya fedha, ukusanyaji wa mapato pamoja na utunzaji wa rasilimali umma, kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na utawala bora, juu ya mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za umma.

Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 112 cha katiba hiyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali

anawajibika kukagua mahesabu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na taasisi zake, ikiwemo mashirika na mamlaka mbali mbali na kutoa taarifa za ukaguzi huo kwa mujibu wa katiba. Kwa mujibu wa kifungu 112(3) cha katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu ya Serikali anawajibika kufanya yafuatayo. Kwanza;

a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina za Serikali, matumizi yake yameidhinishwa na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yametekelezwa ipasavyo basi ataridhia fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa, yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zinazohusika na matumzi ya fedha hizo, na kwamba matumizi yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo. na

c) Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zilizosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahakama zote za Zanzibar, hesabu za tume au vyombo vyengine vinavyohusika na Baraza la Wawakilishi.

Uwasilishaji wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 112(5) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali, atawajibika kuwasilisha taarifa za ukaguzi mara atakapomaliza kufanyakazi ya ukaguzi, taarifa ambayo itaonesha hali halisi na mwenendo mzima wa matumzi ya fedha na rasilimali za umma kwa kipindi kilichokaguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya ukaguzi wa hesabu ni muhimu sana na katika kuimarisha Utawala Bora ambapo nidhamu ya uwajibikaji na matumizi rasilimali za umma huzingatiwa. Kiujumla Utawala Bora katika matumizi ya rasilimali za umma, inahitajia uwazi, uwajibikaji, ushirikishwaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu na usawa wenye kufuata utawala wa sheria.

Kwa kuimarisha dhana Utawala Bora Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali, inaendelea kutoa mchango mkubwa katika kuimarisha uwajibikaji na kukuza Utawala Bora nchini, na kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

Upeo na Madhumuni ya Ripoti za Ukaguzi

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hizo zimekusanya taarifa za ukaguzi wa mahesabu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo taarifa juu ya mapato na matumizi ya rasilimali za umma, zimekaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia 30 Juni, 2015. Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa vya ukaguzi na kujiridhisha, kwamba taarifa zilizotolewa zinaonesha sura halisi ya hesabu zilizokaguliwa. Taarifa hizi zinaonesha kwa muhutasari matokeo ya ukaguzi wa hesabu zilizokaguliwa zinazojumlisha hesabu za mwisho wa mwaka. Kumbukumbu za hesabu na taarifa mbali mbali zinazohusiana na hesabu hizo, ikiwemo mizania ya hesabu, taarifa za mapato na matumizi ya taarifa duniani ya bajeti na mtiririko wa fedha wa mwaka unaoishia Juni 30, 2015.

Utekelezaji wa Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia tathmini ya utekelezaji mapendekezo ya ushauri uliotolewa imebainika kwamba, mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya ukaguzi wa mwaka 2013/2014, yamefanyiwa kazi na kuonesha mabadiliko katika uwekaji na ufungaji wa hesabu katika wizara na taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na kuonesha matumaini ya kuimarika kwa nidhamu ya matumizi, uhifadhi na usimamizi wa fedha na rasilimali za umma.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali, itaendelea kutoa mashirikiano makubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya udhibiti wa rasilimali za umma, na kuhakikisha nidhamu katika utendani na kufuata maadili ya kazi ya ukaguzi kwa lengo la kuleta tija kwa wananchi wa Zanzibar na kupelekea kuongezeka kwa kasi ya maendeleo kwa njia ya umoja, amani, utulivu, uzalendo, upendo na mashirikiano kwa maslahi ya taifa letu.

Taarifa za Fedha za Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali mwaka 2014/2015

Makadirio ya Mapato na Matumizi

Taarifa ya Mapato

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2014/15 mapato yaliyokadiriwa kukusanya kwa jumla ni shilingi 707.8 bilioni. Makadirio hayo yanatarajiwa kutoka katika vianzio mbali mbali, ikiwemo mikopo, misaada ya kibajeti ya washirika wa maendeleo ambapo jumla ya shilingi bilioni 386.8 zilitarajiwa kutoka ndani na jumla ya shilingi bilioni 306 zilitarajiwa kutokana na misaada ya kimaendeleo kutokana na washirika mbali mbali wa maendeleo, pamoja na mikopo ya ndani yenye jumla ya shilingi bilioni 15.

Taarifa ya Matumizi

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitarajia kutumia shilingi bilioni 707.8, ambapo shilingi bilioni 376.5 ni kwa kazi ya kawaida na shilingi bilioni 65.9 kwa kazi za maendeleo, fedha za ndani shilingi bilioni 265.4 kwa kazi za maendeleo kwa fedha za nje kwa miradi na programu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Juni 30, 2015 mapato ya ndani yaliyokusanywa kwa jumla ni shilingi bilioni 354.4 sawa na asilimia 92 ya makadirio yaliyokusanywa, ikiwa na upungufu wa shilingi bilioni 32.4 sawa na asilimia 8 ya makadirio.

Aidha, mapato yaliyotokana na misaada ya kibajeti yalifikia jumla ya shilingi bilioni 232.5. Ukaguzi umebaini kwamba makusanyo ya ndani yameongezeka kwa 2014/15, kwa kukusanya jumla shilingi 354.4 bilioni, ukilinganisha na mwaka wa fedha 2013/14 ambazo makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 330.7, ikiwa ni ongezeko la shilingi 23.7 bilioni sawa na asilimia 7.

Mapato ya kodi yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15 Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 165,996,000,000. Hadi kufikia Juni 2015, makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 143,945,162,000, ambapo ni sawa na asilimia 87 ya makadirio ikiwa ni upungufu wa shilingi milioni 220,508,380 sawa na asilimia 13 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi umebaini kwamba makusanyo yameongezeka kwa mwaka 2014/15, kwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 143,945,162,000. Ukilinganisha na mwaka wa fedha 2013/14 ambapo makusanyo halisi yalikuwa bilioni 136,720,074,000, ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 72,250,880,000, sawa na asilimia 9.5.

Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Mapato Zanzibar ni taasisi iliyopewa mamlaka na jukumu la kukusanya mapato ndani kisheria na inawajibika kukusanya mapato mbali mbali kwa kupitia bodi zilizowekwa na sheria zilizotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15 Bodi ya Mapato Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 171,242,000,000. Hadi kufikia Juni 2015, mapato yaliyokusanywa ni shilingi bilioni 171,863,010,000 sawa na asilimia 94.8, ikiwa ni upungufu wa shilingi bilioni 9,378,990,000, sawa na asilimia 5.2 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi umebaini kwamba makusanyo yameongezeka kwa mwaka 2014/15, kwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 171,863,010,000 ukilinganisha na mwaka 2013/14, ambapo makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 156,572,329,000. Ongezeko hilo la shilingi bilioni 15,990,681,000 sawa na asilimia 9.

Ukusanyaji wa Mapato katika Wizara na Taasisi za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2014/15 wizara na taasisi mbali mbali za serikali, zilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 18,353,000,000. Hadi Juni 2015, makusanyo halisi yalikuwa ni shilingi bilioni 17,564,616,000, ambapo ni sawa na asilimia 95.7 ya makadirio, ikiwa na upungufu wa shilingi milioni 788,384,000 sawa na asilimia 4 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi umebaini kwamba makusanyo yameongezeka kwa mwaka 2014/15, kwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 17,564,616,000, ukilinganisha na mwaka wa fedha 2013/14, ambapo makusanyo halisi yalikuwa ni shilingi bilioni 14,617,095,000, ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 2,947,521,000 sawa na asilimia 20.

Mapato Mengineyo

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2014/15 serikali kwa kupitia msaada wa bajeti ilipata jumla ya shilingi milioni 17,031,883,000, ukilinganisha na makadirio ya shilingi bilioni 40,000,000,000, ambapo ni sawa na asilimia 43 ya makadirio.

Aidha, serikali ilipata hawala za fedha kutoka Benki Kuu ya Tanzania jumla ya shilingi bilioni 3,200,000,000 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi bilioni 3,200,000,000 sawa na asilimia 100 ya makadirio.

Matumizi ya Kazi za Kawaida

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15 serikali ilikadiria kutumia kiasi cha shilingi bilioni 374,905,215,000, kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, ambapo jumla ya shilingi bilioni 348,366,293,000 zimeingizwa na kutumika kwa kazi mbali mbali za kawaida, sawa na asilimia 93 ya makadirio, ikiwa ni upungufu wa shilingi bilioni 26,538,822,000 sawa na asilimia 7 ya makadirio.

Matumizi ya Kazi za Maendeleo

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15 serikali ilikadiriwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 65,900,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, ambapo jumla ya shilingi bilioni 48,764,283,000 na kutumika kwa kazi mbali mbali za maendeleo, sawa na asilimia 71 ya makadirio, ikiwa ni upungufu wa shilingi bilioni 17,135,717,000 sawa na asilimia 26 ya makadirio.

Mambo Yaliyobainika katika Ukaguzi wa Hesabu za mwaka 2014/15

Mhe. Mwenyekiti, haya tu ni baadhi ya mambo ambayo nitayataja hapa chini, kwa sababu kila Mhe. Mjumbe kapewa amepata vitabu viwili, naomba kila mmoja aviangalie vizuri na atizame changamoto zilizojitokeza katika taasisi zetu za serikali.

Katika ukaguzi wa hesabu kwa mwaka 2014/15 ambapo mambo yaliyobainika ni kama haya yafuatayo.

1. Ukiukwaji wa taratibu za manunuzi au ununuzi katika vifaa mbali mbali ikiwemo magari, ujenzi na kadhalika kwa baadhi ya wizara na taasisi za serikali;

2. Malipo yasiyokuwa na vielelezo ikiwemo stakabadhi mbali mbali zinazohusiana na malipo hayo;
3. Ucheleweshaji wa fedha za mapato ya kupelekwa benki;
4. Madeni ya muda mrefu yanayodaiwa wizara na taasisi za serikali;
5. Madeni ya muda mrefu yanayodai wizara na taasisi za serikali;
6. Vifaa vinavyonunuliwa kwa ajili ya matumizi ya wizara na taasisi za serikali kutoingizwa katika daftari la kuhifadhia vifaa ghalani;
7. Fedha za miradi ya maendeleo kutumika kwa ajili ya kazi za kawaida;
8. Fedha za miradi ya maendeleo kutumika kinyume na ilivyokusudiwa; na
9. Fedha zilizoingizwa mwisho wa mwaka wa fedha Juni 2015 kwa baadhi ya wizara na kushindwa kutumika katika mwaka huo na kupelekea fedha hizo kuhaulishwa na kuingizwa katika hesabu za amana za wizara hizo na kukosekana kukaguliwa katika m waka huo wa 2014/15, kutokana na fedha hizo kutokuainishwa katika hesabu za mwisho wa mwaka wa 2014/15.

Mhe. Mwenyekiti, mapungufu hayo yanaweza kurekebishwa kwa vile dosari hizo ni za kiutendaji, ambazo kwa kiwango chake haziwezi kuathiri mwenendo mzima wa hesabu za mwisho wa mwaka na kupelekea kuonesha sura halisi na sahihi ya hesabu hizo.

Shukrani

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kutoa shukrani za dhati kwako Mhe. Mwenyekiti, kwa kufanikisha majukumu yako kwa ufanisi mkubwa. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Baraza la Wawakilishi, ambazo zina umuhimu mkubwa katika maendeleo ya wananchi wa Wanzibar. Kamati hizi zinatoa mchango mkubwa sana katika kujenga na kusimamia misingi ya utawala bora na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali umma.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na umuhimu mkubwa Kamati ya Baraza la Wawakilishi, ofisi imekuwa ikishirikiana na kamati hizo katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na kuhakikisha kwamba taasisi za serikali zinatekeleza malengo yaliyopangiwa, kama ilivyoainishwa katika bajeti zilizoainishwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali (*PAC*), imetoa mchango mkubwa sana katika kusimamia uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma, na kamati hii imekuwa ikishirikiana na Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu katika kufuatilia ripoti zake, na kutoa ushauri wa mapendekezo mbali mbali kwa serikali kwa lengo la kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali hizo.

Mhe. Mwenyekiti, natoa shukrani za dhati kwa Wenyeviti na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati za Baraza la Wawakilishi, kwa msaada wanaotoa kusimamia uwajibika katika kutekeleza majukumu yao ya kisekta. Shukrani za pekee ziwaendee Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali (*PAC*), pamoja na Kamati ya Katiba, Sheria Utawala Bora na Idara Maalum, kwa jitihada mbali mbali wanazochukua katika kutoa maoni yao na ushauri kwa ofisi pamoja na serikali kwa jumla, ambapo ushauri, maoni na michango yao imesaidia kuimarika kwa uwajibikaji na nidhamu ya matumizi ya rasilimali za umma.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, pamoja na wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, kwa kazi na jitihada kubwa wanazochukua katika kusimamia uwajibikaji kwa lengo la kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

Kwa heshima kubwa natoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa jitihada anazochukua kwa kusimamia Utawala Bora nchini na kuhakikisha kwamba nidhamu, uwazi na uwajibikaji katika usimamizi na udhibiti wa fedha na rasilimali za umma zinasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inaendelea kuimarisha utendaji wa kazi kwa kusimamia nidhamu, uadilifu, uaminifu, uwazi na uwajibikaji na kuhakikisha kwamba ukaguzi wa mahesabu unafanyika kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu zilizopo kitaifa na kimataifa, kwa lengo la kutoa ripoti za ukaguzi kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa na kuleta tija kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, itaendelea kuunga mkono jitihada zinazochukuliwa na serikali katika kusimamia uwajibikaji na uwazi wa rasilimali za umma, ili kufikia dhana nzima ya kuimarisha Utawala Bora nchini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*)): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*), juu ya uwasilishaji wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar, kwa kipindi cha mwaka 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote kwa kutujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kuweza kukutana hapa leo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu muhimu kikatiba ya kusimamia serikali na kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar katika kufanya maamuzi muhimu ya kitaifa. Aidha, naomba nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kuzungumzia machache na ya muhimu, yanayohusu uwasilishwaji wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Zanzibar kwa mwaka 2014/2015 kama ambavyo Kanuni ya 43(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016 inavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuweza kuwasilisha hapa Barazani Ripoti hizi mbili, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2014/2015. Ripoti hizi ndio nyenzo kuu za kazi ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC).

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kutoa pongezi na shukurani za dhati kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii ya PAC kwa mashirikiano yao makubwa wanayoendelea kuyaonesha katika utekelezaji wa kazi za Kamati hii. Ni ukweli usiopingika kuwa mashirikiano yao ndio nyenzo pekee inayoifanya Kamati hii kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wao, naomba niwatambue kwa majina Wajumbe na Makatibu hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Mwenyekiti.
2. Mhe. Shaib Said Ali - Makamo Mwenyekiti.
3. Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi - Mjumbe
5. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mjumbe
6. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Mjumbe

7. Mhe. Salma Mussa Bilali - Mjumbe
8. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
9. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa dhati viongozi na watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya za kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za umma zinazotumika kwa shughuli mbali mbali za uendeshaji wa Serikali, licha ya changamoto mbali mbali zinazowakabili. Ofisi hii imefanya kazi kubwa na nzito ya kufanya ukaguzi katika Mawizara, Mashirika na taasisi mbali mbali za Serikali, na kuandaa Ripoti hizi kama ambavyo kifungu cha 112 cha Katiba yetu kinavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti**,** katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya mwaka 2014/2015 ambayo hivi sasa iko mbele yetu inaonesha kuwa aina ya dosari zilizoainishwa katika Ripoti hii hazitofautiani sana na zile zilizoianishwa katika Ripoti kadhaa zilizotangulia. Hata hivyo, tathmini inaonesha kuwa idadi ya Hoja (*queries)* za moja kwa moja katika Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali kwa mwaka 2014/2015 imeonekana kuongezeka na kufikia 42 ikilinganishwa na Hoja 15 zilizobainika katika Ripoti kama hii kwa mwaka 2013/2014. Aidha, Ripoti inaonekana kuainisha maeneo mengi zaidi yaliyofanyiwa ukaguzi ikilinganishwa na maeneo yaliyoainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti**,** miongoni mwa dosari zilizoainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali kwa mwaka 2014/2015 ni ukiukwaji wa taratibu za ununuzi ikiwemo katika ununuzi wa gari Tsh. 46,020,000 katika Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) na ununuzi wa vifaa vya maabara kwa skuli mbali mbali Tsh. 123,918,795 katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Pia, malipo yasiyokuwa na vielelezo Tsh.229,908,131 katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Tsh. 80,232,449 katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na kukosekana kwa maelezo kuhusu matumizi ya Tsh 105,844,100 kwa iliyokuwa Wizara ya Ardhi, Makaazi Maji na Nishati. Vile vile Ripoti imeibua dosari ya uhaulishaji wa fedha Tsh. 58,658,045 kinyume na utaratibu katika iliyokuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti**,** Ripoti hii pia imeainisha masuala ya madeni ambapo hadi kufikia Juni, 2015 Baraza la Manispaa lilikuwa linadaiwa na taasisi mbali mbali jumla ya Tsh. 849,863,497 kutokana na ununuzi wa vifaaa vya usafi, vipuri vya magari, vifaa vya umeme. Aidha, Baraza la Manispaa lenyewe

lilikuwa linazidai taasisi mbali mbali jumla ya Tsh. 102,881,000 hadi kufikia Juni, 2015 kutokana na huduma zilizotolewa na Kitengo cha Mabango cha Baraza hilo. Sambamba na hilo, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kupitia Kituo chake cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti ilikuwa inadai jumla ya Tsh. 41,688,000 ambazo ni ada ya masomo kutoka kwa taasisi na watu binafsi waliopatiwa mafunzo katika kituo hicho.

Mhe. Mwenyekiti**,** pamoja na hayo, Ripoti hii pia haikuacha kuonesha kasoro mbali mbali zilioonekana katika Mradi wa Usarifu wa Mazao (*Agro processing)* Kizimbani zikiwemo baadhi ya fedha za mradi huo kutumika katika miradi mingine na kufanyika kwa sehemu ya malipo ya ufungaji wa mitambo katika jengo hilo la mradi Tsh, 29,450,000 wakati ambapo jengo lenyewe lilikuwa bado halijakamilika ujenzi wake, hali ambayo ilipelekea kutofungwa kwa mitambo hiyo.

Mhe. Mwenyekiti**,** zaidi ya yote hayo**,** Kamati ya PAC imeshtushwa na udhaifu mkubwa ulioainishwa katika Ripoti hii kwenye eneo la ukusanyaji wa mapato kwa kukosekana kwa maelezo na vielelezo vya kuthibitisha makusanyo ya kiwango kikubwa cha fedha yanayotokana na ukodishwaji ardhi *(land lease)* yapatayo Tsh. 3,466,100,000 licha ya kuwa taarifa ya Hesabu ya Wizara iliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kuonesha kuwa iliyokuwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati imekusanya kiwango hicho cha fedha kupitia Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la uwasilishaji wa taarifa za Mapato na Matumizi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kwa mwaka 2014/2015, Ripoti inaonesha kuwa Wizara na taasisi nyingi zimejitahidi kuwasilisha taarifa zao kwa wakati. Hata hivyo, tathmini fupi inaonesha kuwa iliyokuwa Wizara ya Katiba na Sheria ilikuwa ikishindwa kuwasilisha taarifa zake kwa wakati kwa miaka mitatu mfululizo (yaani 2012/2013, 2013/2014 na 2014/2015). Ni imani yangu kuwa kwa uongozi ulio imara na makini zaidi uliopo hivi sasa katika Wizara hii, kasoro hii inaweza kurekebishwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti**,** kutokana na dosari mbali mbali zilizoainishwa katika Ripoti hii, ni dhahiri kuwa kuna haja ya kuweka mikakati madhubuti zaidi na ya pamoja katika kuzirekebisha dosari hizo. Ili mikakati hiyo iweze kuzaa matunda yaliyokusudiwa, ni muhimu kila Afisa Masuuli na kila mtumishi wa umma adhamirie kwa dhati kutekeleza majukumu yake kwa misingi ya uadilifu, uaminifu na weledi. Uadilifu na ubora kwa watumishi wa umma ni

kinga dhidi ya matumizi mabaya ya ofisi za umma na ni moja kati ya njia zinazowawezesha watumishi wa umma kuwa wachapakazi hodari.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kama inavyoonekana, katika masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi wa mwaka 2014/2015 ni pamoja na ukiukwaji wa sheria, taratibu, kanuni mbalimbali, pamoja na udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani. Ukiukwaji huu wa Sheria na taratibu unatia doa na unaiongezea mzigo wa changamoto Serikali yetu ambayo ina majukumu mengi ya kuwahudumia wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti**,** pamoja na kuwa hivi karibuni Baraza lako Tukufu limetunga na kupitisha Sheria mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya 2016 na Sheria ya Usimamizi wa Fedha Namba 12 ya 2016 ili kerekebisha kasoro mbali mbali zilizojitokeza katika Sheria za zamani. Inatupasa tukumbuke kuwa kutunga Sheria na taratibu nzuri katika nchi ni suala moja na kuzisimamia na kuzitekeleza Sheria na taratibu hizo ni suala jengine. Hivyo basi, viongozi katika Serikali wakiwemo Maofisa Masuuli lazima wawe mstari wa mbele katika kuzisimamia ipasavyo Sheria, taratibu na utendaji mzima katika Wizara na taasisi zao, aidha, watendaji nao wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa kufuata kikamilifu sheria na taratibu hizo bila ya kushurutishwa.

Mhe. Mwenyekiti**,** kila aliyepewa dhamana katika utumishi wa umma azingatie misingi ya Sheria, uadilifu, uaminifu na uwajibikaji, si kwa vile anahofu kugundulika akikiuka misingi hiyo bali kwa vile anaamini ndani ya moyo wake kwamba huo ndio wajibu wake. Lengo ni kujenga utendaji katika matumizi ya rasilimali za umma unaozingatia kwa ukamilifu matumizi ya Sheria, taratibu, na uwajibikaji ili tuweze kuimarisha Utawala Bora katika Serikali na nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati ya PAC inatambua na kuthamini sana juhudi na mikakati inayochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kubana matumizi ya Serikali ili kudhibiti vyema matumizi hayo pamoja na kuongeza mapato yatayoweza kuelekezwa zaidi katika kazi za maendeleo. Hata hivyo, Kamati ya PAC inaona ni vyema kwa mikakati hiyo ikaenda sambamba na mikakati ya kupambana kisawasawa na vitendo vinavyoashiria udokozi na ubadhirifu wa fedha na mali nyengine za umma vinavyofanywa na baadhi ya watumishi wakorofi.

Mhe. Mwenyekiti**,** ieleweke kuwa tukifanya hivi pia tutaweza kujisafishia njia ya kukuza uchumi wetu unaotarajiwa kukua na kufikia katika uchumi wa kati.

Katika muktadha huu naomba tujikumbushe maneno ya hekima aliyotuachia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa Awamu ya Pili, Marehemu Mzee Aboud Jumbe Mwinyi katika hotuba yake ya ufunguzi wa Baraza la Wawakilishi, Ngome ya Wananchi, aliyoitoa tarehe 15/1/1980 alisema na naomba kunukuu:

> "Mapambano ya uchumi yanayokabili yanahitaji msimamo sahihi, ujasiri wa kuamua, ufundi wa kupanga pamoja na nidhamu ya utendaji**,** kadhalika uzalendo wa hali ya juu kabisa pamoja na kuaminiana na kushirikiana kidhati".

Mhe. Mwenyekiti**,** licha ya kuwa maneno hayo yalitamkwa katika miaka ya thamanini lakini yanafanyakazi na yana umuhimu mkubwa hadi miaka hii tuliyonayo, kwani ukosefu wa mambo aliyoyaeleza Mzee wetu huyu ikiwemo ukosefu wa nidhamu ya utendaji hasa katika mapato na matumizi ya rasilimali za umma huviza jitihada za Serikali za kuimarisha uchumi wa nchi yetu.
Mhe. Mwenyekiti**,** katika matokeo ya ukaguzi kwa Mawizara, Kamati ya PAC imefarajika kuona kuwa licha ya kubainishwa dosari kadhaa katika Mawizara na Taasisi mbali mbali, Wizara na taasisi zote zilizooneshwa katika Ripoti hii ya mwaka 2014/2015 zimepata Hati za Ukaguzi zinazoridhisha. Hii ni tofauti na Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka 2013/2014 ambapo Wizara na taasisi sita kwa ujumla zilipata Hati Zenye Shaka.

Mhe. Mwenyekiti**,** bila ya shaka haya ni mafanikio makubwa katika kutunza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma ambayo yanahitaji kuenziwa na kudumishwa hasa kwa kuwa maendeleo ya nchi yoyote duniani yanategemea sana uzingatiaji wa uadilifu katika usimamizi na matumizi ya rasilimali za umma na katika utoaji wa huduma bora katika sekta za umma na binafsi.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa upande wa Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali masuala mbali mbali yanaonekana kujitokeza na kuhitaji kufuatiliwa kwa kina ili kuweza kurekebisha hali iliyopo.

Mhe. Mwenyekiti**,** katika eneo la mapato, hali inaonekana ni ya kupanda na kushuka kwa mapato kwa Mashirika tofauti. Kwa mfano, mapato ya Shirika la Magazeti ya Serikali yanaonekana kushuka kutoka Tsh.629,639,622 kwa mwaka 2013/2014 hadi kufikia Tsh. 491,848,991 kwa mwaka 2014/2015 kukiwa na upungufu wa Tsh. 37,790,631 sawa na asilimia 21.

Mhe. Mwenyekiti**,** hali ya kuongezeka kwa mapato imeripotiwa katika Mashirika mbali mbali ikiwemo Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ambayo

mapato yake kwa mwaka 2014/2015 yameonekana kuongezeka kwa asilimia 31. Kwa mnasaba huu basi, Kamati ya PAC inapenda kutoa pongezi za dhati kwa viongozi na watendaji wa PBZ pamoja na Mashirika na taasisi nyengine kwa juhudi na kazi zao nzuri zilizoweza kufanikisha kuongeza mapato katika Mashirika na taasisi zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi, takriban taasisi zote zinaonekana matumizi yao yameongezeka kutokana na sababu mbali mbali ikwa ni pamoja na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji.

Mhe. Mwenyekiti**,** suala la utata wa deni la Shirika la Umeme inalodaiwa na TANESCO limebainishwa katika Ripoti hii ambapo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha usahihi wa deni hilo. Hali hii inaifanya Kamati ya PAC kujiandaa kulivalia njuga vilivyo suala hili ili kujua ukweli hasa ulivyo na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa upande wa Vyuo mbali mbali vya Serikali vilivyoainishwa katika Ripoti hii, uchambuzi wa hesabu za mwisho wa mwaka unaonesha kuwa kuna baadhi ya vyuo huwa vinapata hasara na vyengine huwa vinapata faida. Hata hivyo, Kamati ya PAC inahitaji kulifanyia utafiti wa kina suala hili hasa kutokana na uzoefu kuwa wahusika katika vyuo hivyo wamekuwa wakitoa sababu kuwa misingi na malengo ya vyuo hivyo ni kutoa huduma zaidi na sio kupata faida au hasara.

Mhe. Mwenyekiti**,** baada ya kuzipitia Ripoti mbili hizo tumebaini kwamba zipo baadhi ya Taasisi za Umma hazijakaguliwa takriban mwaka mmoja hadi miaka miwili. Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipotaka maelezo kutoka kwa Mkaguzi Mkuu juu ya utaratibu anaoutumia hata ikawa baadhi ya Taasisi kutokaguliwa ilielezwa kuwa Taasisi hizo hazijakaguliwa kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo ya ubadilishaji wa mfumo wa ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka. Miongoni mwa Taasisi ambazo hazijakaguliwa ni pamoja na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), Shirika la Bandari na Shirika la Bima.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati ya PAC, inazishauri Taasisi hizo kubadilisha mifumo yao mapema ili Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aweze kutekeleza majukumu kama Katiba na Sheria zinavyoelekeza na Ripoti za Ukaguzi wa Taasisi hizo zipatikane kila mwaka kama ilivyo kwa Ripoti za Taasisi Nyengine.

Mhe. Mwenyekiti**,** sambamba na hayo, Kamati ya PAC inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuweka mazingira yatakayomuwezesha Mkaguzi Mkuu wa

Hesabu kuweza kufanya ukaguzi kwenye Mfumo wa Matumizi ya Fedha za Pamoja *(Integrated Financial Management System – IFMS).* Hii ni kutokana na kuwa hivi sasa Mkaguzi huyu anashindwa kuufanyia ukaguzi Mfumo huo kutokana na hitilafu za mtandao za kila mara.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mujibu wa Jadweli la kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, Kamati ya PAC pamoja na mambo mengine imepewa jukumu la kuchunguza na kutoa taarifa juu ya Hesabu ya mwaka ya matumizi ya Fedha za Serikali na Mashirika yake na Hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hivyo, napenda kuchukua fursa hii kulihakikishia Baraza lako Tukufu kuwa Kamati ya PAC itachunguza na kuzifuatilia kwa kina Ripoti hizi na hatimae kuwasilisha Ripoti yake hapa Barazani kama Kanuni za Baraza hili zinavyoelekeza. Ni matumaini yangu kuwa Wizara na taasisi mbali mbali zitaendelea kutoa ushirikiano wao kwa Kamati hii pale ambapo Kamati itapotaka kutekeleza majukumu yake katika maeneo husika.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa kumalizia naomba kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa kunisikiliza kwa makini na kwa utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba yangu hii.

Mhe. Mwenyekiti**,** mwisho kabisa natoa pole kwa wale wote ambao wamepata maafa ya mvua kubwa zilonyesha ikiwemo jimbo langu eneo langu la Panga Tupu nawambia wananchi hao wao na subira waendelee kusubiri waendelee kusubiri mpaka pale Serikali itaona njia gani za ambazo zakutatuwa tatizo hili.
Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa Mhe. Mtumwa Peya kwa uwasilishaji mzuri kwa niaba ya Mwenyekti wa PAC. *(Makofi)*

Mhe. Wajumbe kabla ya kuendelea naomba kidogo nitowe muongozo katika Kanuni zetu. Waheshimiwa Wajumbe tayari wameshaniletea karatasi kuwa wanataka kuchangia. Kwa hivyo nilitaka niwakumbushe katika Kanuni ya 43(3) kauli za Serikali kinachosema kuwa hakutakuwepo na majadiliano yoyote kuhusu kauli yoyote iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii. Lakini wajumbe wanaweza kuuliza masuali, kwa idhini ya Spika, na kumuuliza maswali Waziri aliyetoa kauli hiyo. Kwa madhumuni ya kuwaeweshwa zaidi juu ya maelezo ya kauli hiyo.

Kwa hiyo nilikuwa naomba nitoe muongozo huo kwa Waheshimiwa Wajumbe, maana naona tayari watu wameleta wanataka kuchangia kwa hivyo, Ripoti hii

haitachangiwa ila nitawapa fursa wajumbe, kwa kuuliza maswali katika Ripoti hii. Waheshimiwa Wajumbe nadhani tumeelewana naomba tuendelee nakaribisha masuali kwa kila Mjumbe ambaye anataka kuuliza swali, kwa mujibu wa taratibu tulizoziweka. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kuweza kunipa fursa hii adhimu ya kuweza kuuliza maswali machache kuhusiana na Ripoti hizi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa mwaka fedha 2014/2015. Kwanza kabisa nimpongeza sana CAG kwa kazi kubwa na nzito anayoifanya na kuhakikisha kwamba kila mwaka anatupatia Ripoti za Ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, Maswali yangu yanakuja kama ifuatavyo:

Naanza na hichi kitabu cha Mashirika na Taasisi za Serikali nilikuwa nataka niulize serikali ni lini itafanya tathmini ya kina mashirika yetu haya ili yawe yanaleta tija na sio hasara. Kwa sababu ukiangalia kitabu hiki ukurasa kama wa 13 utaona mashirika mengi kila mwaka hayaleti faida, yana hasara kuwa hasa likiwemo Shirika letu la ZECO.

Sasa ni lini serikali italiifanyia tathmini hasa Shirika hili la ZECO ambalo ni tegemeo la Wananchi wa Zanzibar ili baada ya kuleta hasara iwe inaleta tija. Mdhibiti kagundua mambo mengi mapundufu. Je, serikali imejitapanga vipi kuhakikisha yale mapungufu yaliyoonekana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali yatafanyiwa kazi.

La kwanza anasema daftari la *asset register* halipo, lakini deni lile vile vile la ZECO halina…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Yussuf nadhani nimesema kuhusu muongozo urudi kwenye swali, sasa hivi unachangia. Nimesoma muongozo na nikasema hilo, nimetanabahisha mapema, kwa hivyo rudi kwenye swali lako umuulize Waziri sio maelezo au mchango.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Sawa nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Swali la pili wakati napitia hichi kitabu nimeona kwamba mashirika mengi yamepata hasara lakini yamepata hati tofauti, kuna mengine yamepata hati inayoridhisha kuna mengine yamepata hati isiyoridhisha. Nilikuwa nataka niulize kwa nini kwa sababu yote haya mashirika yamepata hasara lakini yamepata hati tofauti.

Swali la tatu, Ripoti ya Kamati ilikuwa inasema kwamba kuna baadhi ya mashirika hayakufanyiwa ukaguzi likiwemo shirika la Bandari, shirika la Bima pamoja na Shirika la ZSTC, sasa ni lini mashirika haya nayo yatafanyiwa ukaguzi.

Swali la mwisho, kila mwaka tukipokea hivi vitabu kuna mapungufu ambayo yanakuwa yanajirejea kama malipo ambayo hayana vielelezo. Kuna malipo ya ucheleweshaji wa pesa kupelekwa Benki mapato, lakini kuna malipo yasiyokuwa na stakbadhi. Kila ripoti zinazokuja dosari hizi zinajitokeza. Sasa serikali imejipanga vipi kuhakikisha mapungufu haya hayajitokezi tena katika miaka mengine inayokuja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Yussuf, Waheshimiwa Wajumbe nimekuona Mhe. Abdalla Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda kuuliza kidogo kwa upande wa hii ripoti ya CAG husan ile taasisi yenyewe. Lakini kabla ya kuuliza nitaomba ninukuu Kanuni ya Baraza la Wawakilishi ya 96(3) naomba ninukuu...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Diwani, nimekufahamu lakini umesimama na Kanuni hukuomba muongozo, ila umetaka kuuliza swali. Sasa swali lako sijui lipo kwenye hii Kanuni au katika hii ripoti ambayo tunayoijadili.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante swali langu lipo kwenye Kanuni ambalo linahusiana na Afisi ya CAG.

Mhe. Mwenyekiti: Kama swali lipo kwenye Kanuni sisi tunauliza maswali kuhusiana na ripoti iliyoletwa hapa. Kama swali lako litakuwa lipo katika hii ripoti nakuruhusu uulize.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana unajua mimi ni miongoni mwa watu walioifanyia kazi ile ripoti, kuna mambo yalikuwemo ndani ya Kanuni hii ambayo yamekiukwa. Ili nitoe muongozo niweze kufafanuliwa na Baraza lako tukufu. Unaponinyima nisiitumie hii Kanuni na huu ndio tunaamini kwamba ndio msahafu wetu. Samahani. Hii Kanuni ndiyo kitabu ambacho tunachokiamini katika Baraza la Wawakilishi, nafikiri kwamba...

Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, taarifa kidogo. Mhe. Mwenyekiti, huo sio msahafu, kitabu. Msahafu ni kitu kitukufu.

Mhe. Mwenyekiti: Sijakuruhusu Mhe. Nadir Abdulatif tafadhali naomba ukae, sijakuruhusu umepiga meza lakini sijakuruhusu tulikuwa tunazungumza na Mhe. Abdalla Diwani. Mhe. Abdalla Diwani nimezungumza mwanzo kuwa hii kanuni ya 43(3) hakutakuwepo na majadiliano yoyote kuhusu kauli yoyote iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii, lakini Wajumbe wanaweza kwa idhini ya Spika kumuuliza maswali Waziri aliyetoa kauli hiyo hii Kanuni.

Kwa maana hiyo hii imeletwa hapa sio tuijadili, tuulize maswali kwa mujibu wa hii Kanuni ya 43, kwa sababu tayari imeshatolewa ripoti na Kamati imetoa, kwa hivyo bado watarejeshewe tena Kamati ya PAC. Baadaye Kamati ya PAC watakapoleta ripoti ya kuhusiana na ripoti hii iliyoletwa basi tutaijadili ndio hoja yangu iko hapa.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe nawaomba tuulize maswali kama hakuna maswali naomba tuendelee na taratibu nyengine.

Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu, nainuka na Kanuni ya 63, naomba sana Mheshimiwa Mwakilishi afute kauli yake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir, nimekuelewa lakini kuhusu utaratibu sijakusikia na umesimama na hoja yako katika kifungu gani. Sijakuelewa nasema, sijasikia.

Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf: Nainuka nina utaratibu kifungu cha 63, naomba Mheshimiwa Mwakilishi afute kauli yake ya kusema huu ni msahafu wakati hichi ni kitabu. Msahafu ni kitu kitukufu na hichi kitabu kinafutika na kinachanika. Naomba afute kauli yake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadiri nimepokea kuhusu utaratibu kwa hiyo Mwakilishi aliyesema kuwa huu ni msahafu afute kauli yake.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Nafikiri kabla ya kusema nilirekebisha kabla kutoa kauli ile. Nilifuta pale pale kabla ya hata yeye kulifikiria hilo suala baada ya kuona kwamba nimeteleza nikajirekebisha. Nafikiri tayari nimeshafuta kauli yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Abdalla Maulid Diwani, amekuelewa Mhe. Nadir, Mhe. Abdalla Diwani tayari ameshafuta hiyo kauli yake. Waheshimiwa Wajumbe naomba tena twende kwenye hoja, twende kwenye maswali, vyenginevyo tuendelee na taratibu nyengine. Nimwite Mhe. Waziri inaonekana hii ripoti imekubalika. (*Makofi*)

Kama bado naomba Waheshimiwa Wajumbe twende kwa taratibu, tufuate hii kanuni niliyoisoma kuliko hivi. Kwa hivyo kila yule mwenye swali nitaruhusu mwenye swali amuulize Mhe. Waziri basi ndicho kilichokuwepo, vyenginevyo kiti kitafanya maamuzi.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ni miongoni mwa Halmashauri ambazo zinategemewa na serikali ili kuongezea mapato. Vianzio vyake vya mapato, vianzio vyake vya mapato, moja wapo ikiwa ni sehemu ya mapato moja wapoikiwa ni sehemu ya kuchimba mchanga iliyopo Kinazini na mashimo yake kwa sasa hivi yamefungiwa kumefunguliwa eneo langu katika Jimbo langu la Tumbe ambayo eneo lile linafaidisha zaidi wananchi kwa sababu shamba ile iliyopo ni ya wananchi.

Swali langu ni lini mashimo yale ya mchanga yatafunguliwa ili Halmashauri ile iendelee kupata kipato chake ili kuongezea...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Khamis (Doholo) maswali hayo bado wakati wake mtakuja kuhoji itakapoletwa ripoti na Kamati husika. Tusiingie ndani ya hivyo vitabu leo hatujadili. Nawaomba sana Waheshimiwa.

Mhe.Ali Khamis Bakari: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu muongozo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nimekubali muongozo wako, lakini nakuomba ukae. Mhe. Ali Suleiman (Shihata) tuendelee.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Mhe. Waziri kwa taarifa yake nzuri ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2014/15.

Pili nimpongeze Mwenyekiti kwa taarifa yake nzuri aliyoisoma kwa niaba, anafaa Uwawaza kweli imefanya kazi na anastahiki pongezi, nampongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu lipo hapa, nalipongeza Baraza la Manispaa Zanzibar kabla ya mgao yapo Mabaraza matatu katika Mkoa wa Mjini Magharibi ilifanya kazi nzuri ya makusanyo, lakini swali langu lipo hapa. Kwa kuwa Baraza la Manispaa lilikadiriwa kukusanya jumla ya bilioni nne, mia nane, sitini na tatu milioni, laki nane na thamanini saba elfu, mia mbili na hamsini na moja, ukurasa wa 50.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Shihata bado tunarudi kule kule Waheshimiwa, umefungua kitabu unakisoma.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Kuhusu muongozo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani nimekuona na mimi nina haki, umesimama katika muongozo lakini sikuruhusu kutoa muongozo.

Waheshimiwa Wajumbe mtanifanya nifanye maamuzi magumu ambayo nisiyoyatarajia. Mimi sitaki tufike huko kwenye maamuzi magumu. Nimezungumza mwanzo na nikatanabahisha kuhusiana na hii ripoti. Mnafungua kwenye vitabu, tusome hii Kanuni. Waheshimiwa mtoe maswali kwa mujibu wa hotuba aliyoitoa Waziri, siyo kujadili kwenye vitabu. Lakini yale maelezo michango mingi, wewe nenda kwenye swali, ukitoka kwenye swali lako. Lakini ukianza katika hotuba kuna hichi na hichi, wakati wake bado, fursa hiyo mtakuja kuipata Waheshimiwa.Kwa hivyo nakuombeni sana Waheshimiwa turudi kwenye Kanuni, la si hivyo kama hakuna maswali basi tuendelee. Naomba sana waheshimiwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nauliza maswali lakini tarakimu ya fedha ni lazima niitizame, vyenginevyo siwezi kuuliza swali la hewa, hizi naeleza zile fedha tu.

Mhe. Mwenyekiti: Nakufahamu, ila umeanza maelezo, hivi, wapi, wapi, hicho ndicho nilichokisimamia.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Swali langu lipo hapa nasema kwamba Baraza la Manilipaa lilitarajia kukubanya bilioni nne, mia nane sitini na tatu, laki nane thamani na saba, mia mibili na hamsini na moja (4,863,837,251). Lakini katika matumizi yake ilikadiria kutumia fedha hizo hizo katika taarifa ya maoni katika ukurasa 50 bahati mbaya katika makusanya hayo walipata bilioni tatu, milioni mia nane na hamsini na tisa, mia mbili thamani na tano milioni, mia nane na hamsini elfu.

Je, kwa nini walikuwa wakusanye bilioni nne, milioni mia nane na sitini na tatu, laki nane thamani na saba mia mbili na hamsini na moja (4,863,837,251) wakati huo walikuwa wanatarajia kukusanya hizo hizo, walipanga vipi mpango huu kwamba watakusanya hizi halafu tutumie hizi, muelekeo huo unatokaje.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, tumekufahamu sana maelekezo yako, lakini kuna tatizo moja kwa muono wangu. Baada ya

kupata hivi vitabu sisi Wajumbe wengi tumejikita kuviangalia kwa kutafuta hayo maswali kwenye vitabu, sio maswali kwenye hotuba ya Mhe. Waziri. Sasa ushauri wangu, ile hotuba ya Mhe. Waziri angetupatia tukaweza kuuliza maswali kwenye hotuba yake ili tuweze kumuuliza maswali. Kama siyo hivyo maswali itabidi tuulize kwenye kitabu. Naomba muongozo wako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwinyihaji nimekuelewa lakini bado nasema tena kwa mujibu wa hii ripoti PAC ndiyo watakaokuja kushughulika na hii. Kamati ya PAC watakapoipitia hii ripoti, sisi tutalazimika kuja kuihoji wakati wake ukifika, lakini haya maswali tunayotaka kumuuliza Mhe. Waziri yale ambayo *in general* ambayo tunayo sisi hapa. Lakini sio kwa kusema kuwa tumekipitia kitabu, tumekisoma, tumefanyaje. Najua hilo kama mmekipitia lakini bado nalielekeza tena, Kamati ya PAC itakapokabidhiwa hii ripoti, itakapokwenda kuifanyia kazi, watakapotuletea, ndio na sisi tutapata nafasi ya kuuliza, kuhoji kupitia hiki kitabu. Huo ndio muongozo wangu.

Mheshimiwa kuhusu taarifa yako nimeipokea lakini naomba tuendelee. Waheshimiwa Wajumbe naomba tukae. Sasa naona bora nimwite Mhe. Waziri ajibu yale maswali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Muongozo tafadhali, muongozo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani, nakuomba sana, sana, kwa leo nakuomba utulie na nimekufahamu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kukupongeza kabisa kwa kufafanua na kutoa taaluma ya Kanuni, nakupongeza sana. Umeonyesha umahiri mkubwa kwamba kanuni unazielewa.

Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri taarifa niliyoiwasilisha hapa imeulizwa swali na mtu mmoja tu waliobakia walikuwa na maswali mengine.

Waheshimiwa Wajumbe: Wamo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Aliyeuliza swali ni Mhe. Yussuf ndiye aliyeuliza na nitalijibu swali hilo alililiuliza Mheshimiwa. Nataka nitoe maelezo kidogo kwamba Waheshimiwa Mawaziri wote wapo, taasisi zilizohusika zote ziko chini ya mamlaka ya Mawaziri pamoja na mimi. Kila mmoja zile kasoro ambazo zimeonekana kwenye taasisi yake akaziangalie au kwenye shirika lake baadaye Kamati ya PAC itakapokuja watoe mashirikiano kuhakikisha kwamba wanaisaidia Kamati ya PAC ili iweze kupata majibu sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, na sisi Mawaziri mle ambamo tumeonekana kuna kasoro zile katika taasisi zetu tuziangalie tuweze kuzirekebisha kasoro hizo ili zisitokezee tena. Naomba sana suala hili tuliangalie kwa sababu hii ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti zimeelekezwa kwenye Wizara mbali mbali.

Baada ya hayo Mheshimiwa nataka nimuhakikishie Mhe. Yussuf kwamba mashirika yaliyokuwa hayajakaguliwa yatakaguliwa. Vile vile nataka nimuhakikishie kwamba zile taasisi ambazo zimeonekana hati chafu ndiyo wale waliosema kwamba Wakuu wahusika wa taasisi na mashirika hayo, mawaziri na sisi tuliokuwepo hapa. Sote tuzisimamie kuhakikisha kwamba tunazungumza na watendaji wetu ili kuhakikisha kwamba tukikaguliwa tena hati zetu zionekane vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe ripoti imetolewa na Mhe. Waziri sasa naomba niwahoji kuwa ripoti hiyo imepokelewa. Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji, waliokubali ripoti hiyo wanyooshe mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa vile shughuli za leo zilizopangwa zimeishia hapa, sasa naomba niahirishe Baraza mpaka Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

(Saa 12:55 Baraza liliahirishwa hadi Jumatatu
tarehe 15/5/2017 Saa 3:00 asubuhi)